

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 9 Mei, 2022

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadiro ya Mapato na Matumizi ya
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha
2022/2023

MWENYEKITI: Asante, Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali Ofisi ya Rais TAMISEMI, tutaanza na Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara.

Na. 150

Ukarabati wa Shule za Msingi za Zamani - Mwibara

MHE. CHARLES M. KAJEJE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kukarabati Shule za Msingi za Nansimo, Kenkombyo, Kitengule na Namibu zilizopo katika Jimbo la Mwibara?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege Mbunge wa Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Shule 2,147 shule za msingi kongwe nchini ambazo zilianzishwa kabla ya kupata Uhuru mwaka 1961. Hali ya miundombinu ya shule hizo ni mseto zikiwemo zenye hali nzuri na nyingine zenye miundombinu chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeanza kufanya tathimini ya hali ya miundombinu ya shule zote za msingi kupitia mradi wa *BOOST* ili kubaini mahitaji ya ujenzi wa miundombinu mipya ya shule na hali ya uchakavu wa miundombinu iliyopo. Tathimini hiyo imeanza mwezi Aprili, 2022 na itakamilika mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya tathimini hiyo yatatumika kuandaa mpango wa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu ya Shule za Msingi kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026 zikiwemo Shule za Msingi Nansimo, Kenkombyo, Kitengule na Namibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ya shule kongwe za msingi kadri fedha zitakapatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Charles Muguta, swali la nyongeza.

MHE. CHARLES M. KAJEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri na *program* ambayo imeitoa. Ila nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa vile wahenga walisema *seeing is believing*, je, Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili, uko tayari tuongozane, mguu kwa mguu twende tukatembelee hizo shule ambazo nimezitaja ili uone jinsi ambavyo zimechakaa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tayari kwenda na Mheshimiwa Mbunge hata kabla ya Bunge kwisha, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa shule kongwe zinajumlisha pia shule ya Zombo, shule ya msingi pale Jimbo la Mikumi pamoja na Kidodi. Je, Serikali haioni wakati umefika sasa wa kuona namna bora ya kuboresha shule hizi kwa kuzikarabati.

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango ambao tunao sasa hivi miongoni mwa shule ambazo zitafanyiwa ukarabati ni pamoja na hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziainisha.

MWENYEKITI: Ahsante sana tunaendelea, na Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua Mbunge wa Kilindi sasa aulize swali lake.

Na. 151

Hitaji la Gari la Wagonjwa – Kilindi

MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari ya wagojwa katika Wilaya ya Kilindi?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua Mbunge wa Kilindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Kilindi ina gari mmoja la kubebea wagonjwa lililopo kwenye Kituo cha Afya Songe ambalo hutumika kubeba Wagonjwa kwenye Vituo vya Kutolea Huduma za Afya. Uwepo wa gari hilo hautoshelezi kukidhi mahitaji ya halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 itanunua magari 195 ya kubebea wagonjwa ambapo kila Halmashauri itapata gari moja, ikiwemo Halmahsauri ya Kilindi. Ununuzi wa magari haya utaboresha hali ya utoaji huduma za afya kote nchini. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omar Kigua swali la nyongeza.

MHE. OMAR M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanatia moyo kwa wana Kilindi na Watanzania kwa ujumla. Ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa Jimbo la Kilindi lina eneo kubwa la utawala; lina vijiji 102, tarafa nne, kata 21 na vitongoji 611, na gari ambalo linatumika sasa hivi ni gari bovu sana. Je, Serikali iko tayari kutuongezea gari lingine baada ya utaratibu huu ambao upo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa utaratibu huu ambao kila Mbunge anaujua hapa kwamba kila halmashauri itapata magari ya wagonjwa kwa mpango wa COVID-19. Je, ni lini utaratibu huo utakamilika ili wananchi wa Tanzania waweze kupata magari hayo? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Omari Kigua kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwasemea wananchi wa Jimbo la Kilindi. Mimi nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI, tutaendelea kushirikiana naye ili kuhakikisha wananchi wa Kilindi wanapata maendeleo wanayoyatarajia.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ukubwa wa eneo na uhitaji wa gari jingine, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika magari haya yanayonunuliwa, jumla ya magari yote yanayonunuliwa kwa ajili ya huduma za afya katika halmashauri zetu zote, ni magari 407. Kwa hiyo tuna magari 195 kwa ajili ya wagonjwa lakini tuna magari 212 kwa ajili ya ajili ya huduma za usimamizi, chanjo na mambo mengine yanayohusiana na afya. Kwa hiyo, kila halmashauri itakuwa na magari mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba kutakuwa na magari hayo mapya na ni kabla ya Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusiana na lini magari hayo yanakuja, taratibu za manunuzi zinaendelea na mpango wa Serikali ni kuhakikisha ifikapo tarehe 30 Juni, magari yawe yamepatikana; au kama atachelewa sana basi ni Julai, lazima magari yatakuwa yamefika kwenye halmashauri zetu, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Kassinga na Mheshimiwa Anne nimekuona.

MHE. ALLY M. KASSINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya swali la nyongeza. Niipongeze sana Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa mpango wake huu wa kununua magari ya wagonjwa katika halmashauri zetu zote nchini, hongera Serikali. Nikiamini pia kwamba Hospitali yangu ya Wilaya ya Kinyonga, pale Kilwa Kivinje tutapata gari hili. Lakini tuna changamoto kubwa ya vituo vyetu vya afya ambavyo havina magari haya ikiwemo Kituo cha Afya Nanjilinj. Je, kwa upendelea wa pekee Ofisi ya Rais- TAMISEMI itapeleka gari ya wagonjwa Nanjilinj?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

la Mheshimiwa Comrade Ally Kassinga Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Ally Kassinga, kwa kweli anapambana sana kuwasemea wananchi wa Jimbo lake la Kilwa, na sisi tunamhakikishia tutaendelea kuhakikisha tunampa ushirikiano ili wananchi wa Kilwa wapate matunda ya Serikali yao ya Awamu ya Sita. Nimhakikishie, kwamba tunafahamu kwamba Kilwa, nayo itapata gari la wagonjwa, itapata gari la usimamizi, lakini kituo cha Nanjili nakifahamu kiko mbali lakini kinahudumia wananchi wengi. Na katika magari 195 tuna halmashauri 184. Kwa hiyo, tutafanya tathmini na kuona uwezekano wa kungeza gari Kituo cha Afya Nanjilinj. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anne, halafu Mheshimiwa Kakoso.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali; na hili swali naliuliza kwa mara ya pili, na ninamuuliza Mheshimiwa Waziri huyu huyu aliyesimama hapa. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Same, ina majimbo mawali; na majimbo mawili haya yameketi kwenye asilimia 40 ya Mkoa wa Kilimanjaro. Hospitali ya Wilaya iko Magharibi ambako ni mbali sana na Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wakifariki huku Mashariki wanapelekwa Mkoa wa Tanga kwa sababu kituo cha afya ni kimoja na hakijakamilika na hakuna hata *mortuary* mpaka sasa hivi na bado hatuna hata gari la wagonjwa. Mheshimiwa Waziri leo nijibu vizuri nielewe hivi mtaliangalia lini Jimbo langu la Same Mashariki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa uchapa kazi wake ambao umekuwa mfano hapa Bungeni, na wananchi wa Same Mashariki wana mwakilishi bora kabisa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge uliuliza wiki iliyopita swali hili na leo umeuliza na Serikali hii ni Sikivu, tumepokea tutafanya tathmini tutahakikisha kituo cha afya hicho kinaletewa gari la wagonjwa ili wananchi wapate huduma bora za afya, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, Wilaya ya Tanganyika ina tarafa tatu na umbali wa tarafa moja hadi nyingine ni zaidi ya kilomita 130, na jiografia yake ni mbaya. Nilikuwa naomba kuuliza Serikali ni lini itaongeza gari la wagonjwa kwenye tarafa ya Kalema, Kabungu na Mwesi?

MWENYEKITI: tunaendelea, Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa. Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ni wilaya kubwa lakini hizi tarafa ambazo amezitaja na nyingine zinahitaji kupata upendeleo wa makusudi kupata gari la wagonjwa. Niseme kwa ujumla, Waheshimiwa Wabunge wote tutafanya tathmini, tunafahamu jiografia ya halmashauri zetu na majimbo zinatofautiana, tutafanya tathmini kwa maeneo ambayo ni makubwa yanahitaji magari zaidi ya moja. Hivyo, kati ya yale magari yanayoongezeka tutapeleka ikiwemo tathmini ya Tanganyika. Ahsante.

MWENYEKITI. Ahsante sana tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, aulize swali lake.

Na. 152

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Biharamulo Kukosa Fedha

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarejsha fedha Shilingi milioni 204 iliyorudishwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili iweze kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na kanuni zake iliweka utaratibu kwa halmashauri zote nchi, kuomba kibali Wizara ya Fedha na Mipango kwa fedha za miradi zinazotarajiwa kuvuka mwaka wa fedha husika kurejeshwa mfuko mkuu wa Serikali. Maombi hayo yalipaswa kufanyika siku 15 kabla ya tarehe 30 Juni ya mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo haikufuata utaratibu huo. Hivyo, hali hiyo ilisababisha fedha hizo kurejeshwa katika mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilipeleka shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali hiyo, na katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga shilingi milioni 750 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, labda sasa niseme jambo moja, leo ni mara yangu ya tatu nauliza swali hili hili. Mwaka jana kwenye Bunge la bajeti nilijibiwa hivi hivi. Mwaka huu pia Wizara ya Fedha imenijibu kwamba inashughulikia. Ila nimekuwa *disappointed* na majibu ya Serikali kwa sababu wanasema Wilaya ya Biharamuo haikufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina barua hapa ya tarehe 9 Juni, 2020, *copy* ninayo na ninaamini kila sehemu ipo. Nina barua hapa ya tarehe 20 Agosti, 2020 *copy* ninayo na barua ipo. Sasa kinachoshangaza ni kwamba, majibu niliyopewa na Wizara hii hii mwaka jana ni tofauti na majibu ninayopewa leo. Nilikuwa naona kwamba tumeshaenda mbele, lakini majibu nayojobiwa leo wananirudisha nyuma tena. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza, naomba Serikali inipe majibu hapa wananchi wa Biharamulo wakiwa wamesubiria hospitali kwa muda mrefu.

Ni lini fedha hii inapelekwa? Yaani lini siyo nyuma wala mbele lini, *date*, kabla ya mwisho wa bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili tuna pesa milioni 376 kwa ajili ya vifaa tiba ya hospitali hii. Sasa, leo ni mwezi wa tano, mwaka wa fedha unaisha. Kwa hiyo tusiletewe hii fedha mwezi wa sita katikati tukaambiwa inatakiwa itumike kwa haraka. Pamoja na hii nijue fedha ya vifaa tiba inakuja lini, na utaratibu wake ukoje kama kama inachelewa tunairudisha au tunabaki nayo? Majibu mawili tu.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya kazi kwa kufuata kumbukumbu ambazo zinaoneshwa katika mafaili yetu lakini katika *document* mbalimbali za Serikali. Na sisi tumefuatilia Wizara ya Fedha na Mipango; pamoja na kwamba Mheshimiwa Mbunge una hizo barua inawezekana ziliandikwa lakini hatuzioni Wizara ya Fedha na Mipango, na suala lilikuwa sio kuandika barua ilikuwa barua zifikishwe Wizara ya Fedha na Mipango.

Kwa hiyo, kama waliandika kwa ku-*back date*, ili kuweza kutengeneza mazingira hayo sisi hatujazipata hizo, na tungezipata nikuhakikishie Serikali Sikivu ingezifanyia kazi. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunachosema hapa ni sahihi na tunaendelea kusema vitu sahihi katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na lini fedha hizi zinapelekwa katika mwaka huu wa fedha tayari mmepeata milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Biharamulo. Mwaka ujao wa fedha mmepeata milioni 750 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Kwa hiyo, hapa ni wazi kwamba Serikali inaendelea kupeleka fedha na hospitali inaendelea kujengwa. Hitaji la wananchi ni hospitali na Serikali ina *commitment* kubwa kuhakikisha hospitali inaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na milioni 376 za vifaa tiba utaratibu upo wazi tunatepeleka fedha Bohari Kuu ya Madawa (*MSD*) na itanunua vifaa vile ambavyo imeorodheshwa na halmashauri vitaletwa kwa ajili ya huduma hizo. Nikuhakikishie tu, kwamba *MSD* inakwenda vizuri sana, vifaa vitakuja huduma zitaendelea pale Biharamulo.

MWENYEKITI: Ahsante sana, nimekuona Mheshimiwa Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti; iko dhamira ya Serikali ya kujenga hospitali za halmashauri

28 katika bajeti ambayo tunaimaliza sasa. Je, lini hospitali hizi zitapelekewa fedha, ikiwemo hospitali ya Halmashauri ya Itigi?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Massare, Mbunge wa Manyoni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali zote za halmashauri zote ambazo zimeanza ujenzi na vituo vyote vya afya ambavyo vimeanza ujenzi kwa fedha ya Serikali mpango wa Serikali ni kuendelea kupeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali hizo. Ndiyo maana kwenye mwaka ujao wa fedha tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali zile 59, ikiwemo hii ambayo Mheshimiwa Massare ameisema. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Dkt. Kabati kwa niaba.

Na. 153

Mpango wa Serikali Kurudisha Uoto wa Asili Katika Milima ya Iringa

MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusni wa kurudisha uoto wa asili wa milima ya Iringa ili kuendelea kutunza mazingira yake na vyanzo vya maji?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Maiznigra, naomba Kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imebaini kuwepo kwa uharibifu wa mazingira unaotokana na uvamizi wa wananchi wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye milima na vyanzo vya maji katika Wilaya ya Iringa Mjini pamoja na Wilaya nyingine Mkoa wa Iringa. Kutokana na changamoto hiyo, Mkoa wa Iringa umeanzisha programu ya upandaji miti kwenye maeneo yaliyoharibiwa ambapo kila Kata imepanda miti 1,000 kwa mwaka ili kuokoa maeneo yaliyoharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, programu hii imeimarishwa zaidi na uzinduzi wa kampeni ya ‘Soma na Mti’ iliyozinduliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo tarehe 25 Januari, 2022 katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Iringa. Kampeni hii imehamasisha shule za Msingi na Sekondari za Mkoa wa Iringa kupanda miti takribani 27,656 katika maeneo mbalimbali ikiwemo shule vyanzo vya maji, mabonde, miteremko ya milima na kandokando ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha mazingira ya milima na vyanzo vya maji katika Mkoa wa Iringa yanastawi Ofisi ya Mkoa wa Iringa inaendelea kuotesha vitalu vya miche Laki Tatu kila mwaka na kuwapatia wananchi wa mkoa wa Iringa kuipanda katika maeneo yao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya

nyongeza. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna vikundi ambavyo vimekuwa vikijishughulisha na utunzaji wa mazingira na yeye mwenyewe amekiri hata wanafunzi wameendelea kufungua *program* zao. Changamoto kubwa vikundi hivi vinakuwa vina ukosefu wa fedha ili viweze kufanya vizuri zaidi.

Je, Serikali inawasaidiaje, vikundi hivi viendeleo kupanda miti mingi na kuendelea kutunza mazingira ambayo wanayaishi?

Swali la pili, ili kupunguza shughuli za kibinadamu kuzunguka milima na vyanzo vya maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha kufanya shughuli zingine kama za ufugaji, uvuvi, katika maeneo ambayo wanazunguka wananchi?

MWENYEKITI: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa vikundi mbalimbali ambavyo vinahitaji kusaidiwa, lakini tunajiridhisha na kuangalia umuhimu wa vikundi hivyo na kwa kiasi gani wanasaidia na wao katika kuimarisha mazingira ndani ya milima lakini na vyanzo vya maji. Serikali ipo tayari kabisa kuwasaidia vikundi hivyo kwa ajili ya kuimarisha mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, namna gani tutawezesha, tutawezesha kwa kuwapatia taaluma mbalimbali na kuwaita katika mikutano yetu ili kuwapa taaluma kwa ajili ya kuimarisha mazingira ndani ya nchi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shally nimekuona, halafu Mheshimiwa Asha Juma.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tatizo lililo kwenye milima ya Iringa linafanana kabisa na tatizo lililoko tambarare ya Mlima wa Kilimanjaro kwa ajili ya mabadiliko ya tabia nchi. Je, Serikali itaungana lini na wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro, ambao wako tayari sana kurejesha uoto huo kwa kuotesha miti katika vihamba vyao, hususani miti ya matunda? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lake ni kweli tunajua kwamba wanawake ama vikundi mbalimbali wakiwemo wanawake, wanaimarisha sana suala la mazingira kwa upandaji miti, pamoja na na miti ya matunda. Serikali inaahidi kutoa motisha kwa wale ambao watafanya vizuri kwenye kampeni yetu kapambe ambayo itamalizika tarehe 30 Juni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Juma nilikutaja.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa uharibifu huu unaofanyika kwenye milima, uko vilevile kwenye fukwe za bahari na zile sehemu ambazo bahari inaungana na mito. Mikoko inazidi kukatwa, kila kukicha na hivyo kuharibu mazingira na sehemu za kuzalia viumbe vya majini.

Je, Serikali sasa itakuja na *program* gani ya kuongeza hamasa katika kupanda mikoko katika sehemu hizo ili kunusuru mazingira hayo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha maarufu kwa jina la 'Mshua' kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango mkakati ambao wananchi wote ambao wanasaidia kupanda mikoko kando kando ya bahari, wanakuwa na taaluma maalum lakini wanapewa motisha. Kwa mfano, Bagamoyo, Zanzibar, ziko sehemu ambazo tayari wameshapanda mikoko na wale ambao wamepanda mikoko *well* na ikawa inahuika, basi Serikali tunawapa motisha na kufuatilia siku hadi siku. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika Wilaya ya Rungwe kuna sehemu ya chanzo cha maji cha Kijungu ambayo inapeleka kwenye daraja la Mungu maji yanayoenda kwenye Mto wa Kiwira. Serikali imeacha kwa muda mrefu sana kuweka mazingira na kuhakikisha chanzo hiki kinakuwa salama na kuendelea kuwa historia ya Wilaya ya Rungwe.

Je, ni lini mtapeleka fedha na kuhakikisha mnalinda eneo lile linakuwa salama na linaendelea kuwa kivutio kwa Watanzania na wageni wanaokuja pale?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu la Mheshimiwa Sophia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ambayo imewekwa ya ofisi yetu basi sehemu hii ambayo umeitaja

Mheshimiwa tumeichukua na ndani ya bajeti yetu ipo na tutatekeleza mara baada tu ya kikao hiki cha bajeti. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, litaulizwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na. 154

Hitaji la Chuo cha VETA Magu

MHE. STANSLAUS S. MABULA - K.n.y MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA aliluliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Magu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kuwezesha upatikanaji wa fursa za ujuzi na stadi mbalimbali za maisha kupitia elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika Mikoa na Wilaya zote nchini. Kutokana na nia hiyo, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa ujenzi wa Vyuo vya VETA kwa awamu katika Mikoa na Wilaya mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Magu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi ambacho Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Magu na maeneo mengine, wananchi wa Magu wanashauriwa kutumia Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Mwanza pamoja na Vyuo

vingine vya *VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo jirani kwa ajili ya kupata elimu na mafunzo ya ufundi. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stanslaus Mabula swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa sababu Serikali inao mpango wa kutafuta fedha na kuhakikisha vyuo hivi vinajengwa. Wilaya ya Magu imeshatenga zaidi ya hekari 30, ikitegemea Serikali ipeleke fedha kwenye eneo hili na wananchi waweze kufaidika na vyuo hivi vya *VETA*. Sasa Serikali tunaomba *commitment* yake kwamba itakapopata fedha, Wilaya ya Magu iwe ya kwanza kwa sababu hata kule Kwimba, wanajenga kituo ambacho kina miaka miwili leo na hakijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na Serikali kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka kwenye ujenzi wa vyuo vingi vya *VETA*, vyuo vingi vimekuwa havina vifaa vya kufundishia na matokeo yake wanafunzi wengi wanajifunza kwa *theory* peke yake.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kila Chuo cha *VETA* kinapoanzishwa kilichopo kinakuwa na vifaa vyote stahiki kwa ajili ya kufundishia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika sera yetu ya Serikali kwamba tutakwenda kujenga Chuo cha *VETA* katika kila Wilaya na Mkoa katika Taifa letu. Nimuondoe wasiwasi

Mheshimiwa Mbunge na kumpongeza vilevile kwa ufuatiliaji wa karibu, iwapo Serikali itapata fedha, basi kipaumbele cha kwanza kitakuwa katika Wilaya hiyo ya Magu na Wilaya nyingine ambazo tayari zimeshatenga maeneo kwa ajili ujenzi wa vyuo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimtoe wasiwasi vilevile katika eneo hili la pili la vifaa. Kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge katika awamu ya kwanza tunakwenda kujenga Vyuo 25 katika Wilaya 25 mbalimbali nchini, tayari Vyuo hivyo viko mwishoni kabisa katika kumalizika kwake na tunaamini ifikapo Julai, vyuo hivi vinaweza kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili Serikali tayari imeshatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya vyuo hivi ili basi vitakapofunguliwa pamoja na ufundishaji wa nadharia lakini ufundishaji wa vitendo uwe umepewa kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi tayari Serikali inafanyia kazi jambo hili na fedha tayari imeshatengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kihenzile nimekuona.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi wanayofanya ya kuhamasisha *VETA* katika nchi yetu.

Nataka kufahamu tu kwa ufupi ni lini Serikali inakwenda kutekeleza ujenzi wa *VETA* pale Mufindi, ikizingatiwa kwamba sasa tarehe 29 Aprili, Baraza la Madiwani limeamua *VETA* ikajengwe Nyololo, lini utekelezaji wake unafanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kihenzile, alikuwa anafuatilia suala hili kwa karibu. Mheshimiwa Kihenzile wewe mwenyewe ni shahidi nadhani tumeshawahi kuonana siyo mara moja, siyo mara mbili na umeshawahi kuja ofisi zaidi ya mara moja kwa ajili ya suala hili. Kwa vile tayari mmeshapitisha kwenye Baraza lenu la Madiwani ambalo ndilo lenye mamlaka ya kupanga wapi chuo hiki kijengwe. Nikuondoe wasiwasi iwapo Serikali itapata fedha, kipaumbele kitakuwepo katika maeneo haya ya Mufindi kwa sababu tunajua kule kuna shughuli nyingi sana ambazo zinahitaji masuala haya ya ufundi kuweza kuzingitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nikuondoe wasiwasi nalo hili tunalifahamu tutalitilia mkazo kwa karibu zaidi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 155

Kuboresha Huduma za Afya kwa Wazee

MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y MHE. ZAYTUN S. SWAI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma za Afya kwa Wazee hasa wa Mkoa wa Arusha kwa kuwapatia dawa kupitia mfumo wa bima tofauti na iliyopo sasa?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishatoa maelekezo kwa wasimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya kuwa wazee wasio na uwezo na waliotimiza vigezo wapewe huduma za Afya wakiwa nje na ndani ya mikoa yao. Aidha, Serikali ipo kwenye hatua ya ukamilishaji wa Muswada wa Bima ya Afya kwa wote utakaowezesha makundi yote kupata huduma za afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mussa maswali ya nyongeza.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo ya Serikali lakini bado kuna changamoto kubwa sana ya wazee kupata huduma ya afya kwenye vituo vyetu vya afya, hususan hospitali zetu za rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niombe Serikali kuna changamoto kubwa sana, umefika wakati wa kutoa tamko rasmi kabisa kwamba wazee hawa watibiwe bure na ikionekana kuna changamoto yoyote kwenye hiyo hospitali hatua zichukuliwe mapema.

Je, Serikali inatoa tamko gani sasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge amelezea vizuri na tunapokea ushauri wake, Waziri wa Afya kwa kushirikiana na Waziri wa TAMISEMI, watatoa maelekezo mahususi kwa maandishi kwa ajili ya hilo kutekelezwa kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zacharia Issaay nimekuona.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Tatizo la huduma bure kwa wazee, akina Mama na Watoto limekuwa ni changamoto kubwa sana katika nchi yetu, na kwa kuwa wote tulioko hapa ni wazee watarajiwa leo, kesho, keshokutwa na mtondo *go*.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kutoa waraka wa wazi kwa ajili ya jambo hili la huduma katika makundi niliyoyataja?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tunapokea ushauri wa Mbunge na labda niseme tu kidogo kwamba, kwa mfano tunazungumzia tu wazee walioko kwenye mfumo ambao ni wastaafu 149,000 ukiwaangalia sasa hivi kwa mwaka tu wanatumia Biloni 61 kwenye kupata huduma za afya ambayo ni asilimia 82 tu wao ndiyo wagonjwa. Kwa maana hiyo, ukizungumzia wazee wote kwenye nchi nzima nalo ni tatizo kubwa na nakubaliana naye kwamba inahitajika hela nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kama ambavyo nimesema swali la kwanza la msingi tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba hayo mambo yanafuatiliwa kwa ukaribu lakini tunawaomba wenzangu Wabunge na sisi tufatilie kwa karibu kuhusu wanavyohudumiwa wazee na mkiona kwamba hawahudumiwi tupaze sauti kwa pamoja, lakini sisi tutaelekeza sheria na kusimamia na kuwaadhibu ambao wanaacha kutekeleza maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Lugangira nimekuona na Mheshimiwa Kassim ajiandae.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee wa Mkoani Kagera walipewa vitambulisho ambavyo vinawaruhusu kwenda

kupata matibabu bure. Lakini vitambulisho vile havitambuliki pale ambapo wanakwenda kwenye hospitali au vituo vya afya. Vilevile wakiandikiwa dawa, huwa wanaandikiwa dawa ambazo bado wanaambiwa hawawezi wakapewa pale hospitali au kituo cha afya, inabidi wakanunue nje.

Je, Serikali ina mpango gani kudhibiti hayo maeneo mawili? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikia ni Mzee mwenye kitambulisho chake, maana yake ni mzee ambaye tayari ameshatimiza vigezo vyote ambavyo vinatakiwa apate huduma. Kwa hiyo, kimsingi anatakiwa apate huduma. Lakini kuna hilo tatizo sasa kwamba anapewa huduma lakini anapofika dirisha la dawa, dawa inayohitajika kupata haipatikani haipo kwenye dirisha la dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesikia hapa nyuma tukiwa tunazungumza masuala ya *MSD* na upatikanaji wa madawa kwenye vituo vyetu. Nguvu nyingi sasa tunaelekeza kuhakikisha hakuna dawa inayokosekana kwenye vituo vyetu ili wazee wetu waliotimiza vigezo wakienda kwenye dirisha la dawa wapate dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Jumamosi tulikuwa na Wabunge wenzetu wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa ajili ya Muswada wa Bima ya Afya kwa wote. Sasa tutaenda kutoa semina kwa Wabunge wote likija Bungeni basi tulisimamie hilo kwa sababu ndiyo litakuwa suluhu la kudumu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kassim nimekuona.

MHE. KASSIM HASSAN HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huduma hizi za Bima ya Afya upatikanaji wa dawa kwa upande wa Zanzibar zimekuwa za chini sana.

Je, ni lini Serikali itaenda kuboresha huduma hizo ili watu wapate dawa katika hali ambayo itakuwa ni ya kawaida?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe tu Mbunge, wakati wa sisi kupitisha Muswada wetu wa Bima ya Afya kwa watu wote, wote kwa pamoja tushirikiane kuweka input nzuri ambayo mwisho wa siku italeti suluhu ya kuduma bila tena kuona wazee wanarudi kule kule ambako hatukupenda warudi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa Mbunge wa Mtambwe.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa. Sasa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe.

Na. 156

Kupambana na Magonjwa Yasiyoambukiza

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na magonjwa yasiyoambukiza?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza ni kutoa elimu kinga, kusomesha Madaktari Bobezi kwenye eneo hili pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba vya teknolojia ya juu katika utambuzi na tiba ya magonjwa yasiyoambukiza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khalifa Mohamed, swali la nyongeza.

MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jawabu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; Magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza kwa kweli yanaongezeka kila uchao. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2016 kulikuwa na wagonjwa takribani milioni nne na kumi na nane elfu, lakini kufika mwaka 2020 kumekuwa na wagonjwa wasiopungua milioni nne na laki nane. Magonjwa haya yanagharimu Serikali kupitia Wizara ya Afya takribani asilimia 20 ya bajeti yake na vifo takribani asilimia 33 ya vifo vyote. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba, wakati sasa umefika magonjwa haya kuyaundia Tume Maalum ambayo itayashughulikia kama vile *TACAIDS*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; miongoni mwa magonjwa haya yasiyoambukiza ni saratani ambayo nayo inaua watu wengi sana na pia inagharimu pesa nyingi sana kwa kuagiza dawa kutoka nje. Je, Waziri haoni wakati sasa umefika wa kuwa na kiwanda ambacho kitazalisha mionzi tiba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumjibu swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge anashauri kwamba tuanzishe tume kama ya *TACAIDS* kwa sababu magonjwa haya yanaonesha kila mwaka yanaongezeka na yanakuwa ni tatizo kubwa kwenye nchi yetu. Tatalifanyia upembuzi yakinifu wazo lake, lakini kikubwa ni kwamba ni sisi kuongeza nguvu zaidi kwenye kuelimishana hasa haya magonjwa yasiyoambukiza, namna *life style* na mambo

mengine ili kupunguza idadi ya watu ambao wanapata matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuongeza bajeti na kubwa zaidi kwenye eneo hili ili elimu iwafikie watu wengi lakini watu wengi zaidi wapate huduma bila bughudha yoyote. Maana yake ukianzisha taasisi wakati mwingine tunarudi kule kule, fedha nyingi zinaishia kwenye masuala ya utawala badala ya kumfikia mgonjwa husika. Kwa hiyo nafikiri ni kuongeza nguvu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ambalo kimsingi linaonyesha ni namna gani Serikali ilivyo *serious* kwenye eneo hili, ni suala alilosema kwamba kiwanda cha kutengeneza mionzi dawa. Kiwanda cha kutengeneza mionzi dawa kama tulivyo sema hapa kwa Afrika ni nchi nne tu zilikuwa na uwezo na kiwanda hicho na sasa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ndani ya mwaka mmoja amewezesha na tayari hicho kiwanda kipo na mwezi wa sita kinaenda kuanza kazi rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi na ukiangalia maana yake ni nini? Sisi kwa Afrika sasa Rais wetu ametufikisha mahali, katika nchi tano ambazo zina kiwanda cha kuzalisha mionzi dawa na sisi tuko. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nafikiri eneo hilo linaenda vizuri na hatuna haja ya kutengeneza taasisi. Unajua watu wetu kwenye masuala ya utawala fedha nyingi badala ya kwenda kwa mgonjwa zinaweza zikaishia kwenye masuala ya utawala.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma Toufiq, nimekuona.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Nataka kufahamu nini mkakati wa Serikali wa kupeleka dawa za magonjwa yasiyoambukiza katika ngazi ya zahanati?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali moja ilikuwa ni kupatikana vile vitu ambavyo huduma hiyo inaweza ikafanyika na mmeona sasa hivi kwamba karibia kila jimbo kila mahali kuna ujenzi unaoendelea kwa ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na mambo mengine. Kikubwa sasa hivi na kwa ajira iliyopo sasa hivi utaona sasa hivi Madaktari wenye *level* ya digrii sasa hivi wameshafikishwa mpaka vituo vya afya na dawa hizo zinaenda kutolewa kwa ukaribu zaidi. Kwa hiyo Serikali ina mkakati kuwa, tunapomaliza hivi vituo wakati tunaweka vifaa, tunaweka madawa, lakini wataalam watapelekwa wenye uwezo wa kuwatibu watu wenye matatizo hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Faharia Shomari, nimekuona.

MHE. FAHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa maradhi yasiyoambukiza kama sukari na presha, ushatumia dawa kwa muda mrefu au uliugua kwa muda mrefu, lakini kila ukienda kupima inaonekana *normal*/kwa sababu unatumia dawa kwa wakati. Je, inaweza kupunguza dawa kutumia ili niepushe kupata maradhi mengine wakati tayari maradhi haya yako *normal*?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge ambalo ni lizuri. Nafikiri nisingetoa ushauri wa kijumla kwa sababu kila mtu anakuwa na hali halisi anapofika kwa Daktari. Nashauri jambo lolote unalotaka kufanya inapofikia mahali una shida ya presha au sukari, usiamue kijumlajumla, amua baada ya kufika kituo cha afya, kupewa vipimo na Daktari mwenyewe kwenye eneo hilo na kukushauri.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 157

Vijiji Vilivyosambaziwa Umeme wa REA – Kagera

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU aliuliza:-

Je, ni vijiji vingapi havijapatiwa umeme wa REA na nini mpango wa Serikali kusambaza umeme kwenye vijiji vyote vya Mkoa wa Kagera?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera una vijiji 662, ambapo kati ya hivyo, vijiji 139 havijafikiwa na miundombinu ya umeme. Vijiji vyote 139 vilivyobaki vitapatiwa umeme kupitia utekelezaji wa Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu – Mzunguko wa Pili unaoendelea. Mkandarasi ambaye ni *Joint Venture* wa kampuni za *M/S JV Pomy Engineering Company Limited* na *Qwihaya General Enterprises Company Limited* ndiyo wanaotekeleza mradi huo kwa Mkoa wa Kagera. Gharama ya mradi ni Shilingi Billioni 34.078.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa kilomita 812 za njia za umeme msongo wa kilovoti 33, ufungaji wa mashine umba 176, ujenzi wa kilomita 139 ya miundombinu ya usambazaji ya msongo wa voti 400 na uunganishaji wa wateja wa awali wapatao 3,058. Utekelezaji wa mradi umeshaanza kwa mkandarasi kukamilisha upimaji na usanifu wa kina na kuanza uagizaji wa vifaa vya utekelezaji. Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2022.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bernadeta Mushashu.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza. Hadi sasa maeneo mengi katika Mkoa wa Kagera ambayo yamesambaziwa umeme wa *REA* umeme umefika tu kwenye ngazi ya vijiji haukuteremka chini. Swali la kwanza, je, ni lini sasa madi wa ujazilizi *densification* itaweza kuanza Mkoani Kagera ili vijiji vyote sasa na maeneo yote yaliyorukwa na vitongoji yaweze kupatiwa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika Mkoa wa Kagera kwenye Manispaa ya Bukoba tunazo Kata kama Kahororo, Buhembe, Nshambya, Nyanga, Kagondo, Kibeta, Kitendaguro na Ijuganyondo ambavyo pamoja na kwamba kata hizo ziko kwenye Manispaa ya Bukoba lakini zimekaa kama vijiji. Je, ni lini sasa Serikali itaanzisha mradi wa *Peri-Urban* ili sasa vijiji hivi au mitaa hii inayofanana na vijiji iweze kupata umeme wa *REA* kwa bei nafuu?

MWENYEKITI: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bernadeta Kasasabago Mushashu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwenye awamu ya kwanza upelekaji wa umeme vijijini tumefika hasa kwenye *centres* za yale maeneo na ni kwa sababu ya fedha iliyokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA III round II* peke yake ina shilingi trilioni moja na bilioni mia mbili na hamsini kwa ajili ya kufikisha umeme kwenye vile vijiji vyote ambavyo havikuwa na umeme. Azma na nia ya Serikali ni kuhakikisha kila mtu anapata umeme kwenye eneo lake na tayari nia hiyo imeanza. Tayari uko mradi wa ujazilizi tunaita *Densification One* ambao unaendelea katika baadhi ya

maeneo yetu, lakini tumemaliza tayari upembuzi na kupata wakandarasi, tunaamini kufikia Julai *densification 2(b)* itaanza, lakini kufikia kwenye Oktoba *densification 2(c)* itaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hii haitaweza kumaliza kwa sababu katika hizi *densification* tuna vitongoji karibu 5,000 na zaidi kidogo. Mnakumbuka hapa tayari Bungeni Mheshimiwa Waziri amesema kwamba tunatafuta mkakati mkubwa wa kuweza kupata fedha nyingi karibia trilioni sita kwa ajili ya kupeleka sasa umeme kwenye vitongoji vyote vilivyobaki nchini ambavyo havina umeme. Kwa hiyo kadri pesa inavyopatikana vitongoji vitazidi kupelekewa umeme kwa kadri Serikali inavyozidi kujipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili la *Peri-Urban*, nimshukuru Mheshimiwa Bernadetha kwa kuulizia kuhusu Jimbo la Bukoba Mjini, makofi yalikuwa mengi, swali sikulisikia vizuri, lakini naamini alichokizungumzia ni *peri-urban* na tayari Serikali imeshatangaza na imefikia hatua za mwisho za kupata wakandarasi wa kupeleka umeme katika maeneo ya mijini lakini yenye uso wa vijiji kama alivyozitaja hizo kata saba za Jimbo la Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mikoa mingine kama tisa katika awamu hii ya *peri-urban* nayo kufikia Julai tunaamini mradi huu utaanza kwa ajili ya kufikisha umeme katika maeneo haya kwa ajili ya kupata umeme kwa gharama nafuu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndaisaba.

MHE. NDAISABA G. RUHORU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba sasa Serikali inijibu, ni kwa nini mkandarasi wa *REA* Ngara amepotea *site*, haonekani kwa takribani kipindi cha miezi mitatu? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya upelekaji wa umeme vijijini iko na awamu tofautitofauti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kuna upembuzi yakinifu, ku-*survey* yake maeneo, uagizaji wa vifaa na hatua ya mwisho ya uwekaji wa miundombinu yenyewe. Maeneo hayo na mazingira hayo ya hatua hizo yanaweza kufanya mkandarasi asionekane *site* kwa muda na hasa pale anapokuwa kwenye hatua ya kuagiza vifaa. Naamini maeneo mengi wengine vifaa vimefika, wengine bado, kwa hiyo sehemu ambapo hajafika, naamini itakuwa labda alichelewa kwenye kuagiza vifaa, lakini vifaa vitafika, kwa sababu maelekezo yetu ni kabla ya Desemba mwaka huu miradi iwe imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwaelekeza wakandarasi wote kuendelea na kazi katika *site* zao kulingana na *schedule* walizoziweka na vifaa vilivyopo ili tuweze kufikia *deadline* ya Desemba kuweza kufikisha umeme kwenye maeneo hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi, nimekuona.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kata ya Mbaramo na Shagayo katika Jimbo la Mlalo bado hakuna hata kijiji kimoja kimesambaziwa umeme. Nataka kujua, ni lini Serikali itanza usambazaji wa umeme katika kata hizo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga unao wakandarasi watatu wanaopeleka umeme vijijini na katika Jimbo lake yuko Mkandarasi anaitwa *Dem Electric* ambaye

anapeleka umeme katika maeneo hayo. Nafahamu kwamba mkandarasi huyu anajitahidi kufanya kazi zake vizuri na atakuwepo kwenye maeneo ya kazi, pengine ameanzia eneo lingine ili aje amalizie kwenye hayo maeneo ya kata alizozisema za Mbaramo na Shagayo kama nitakuwa nimezitaja vizuri. Nichukue nafasi hii kumwelekeza yeye pamoja na wakandarasi wengine wagawanye magenge wanayotumia katika kufanya kazi ili kila eneo la Mbunge liweze kuonekana likiwa linafanyiwa kazi kama ambavyo walienda wakari potu wakaanza kufanya kazi za utekelezaji katika maeneo hayo na eneo hilo liwe mojawapo la kuhakikisha kwamba wanatoka kwenye maeneo waliyofikia sasa kwenda kwenye maeneo mengine ili kufanya kazi na kukamilisha kazi kwa wakati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha, nimekuona.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa Jimbo la Hai kuna changamoto kubwa sana ya uchakavu wa miundombinu, lakini kumekuwa na maombi ya muda mrefu sana ya wananchi tangia mwaka 2008 mpaka sasa hivi hawajaunganishiwa; na kwa kuwa tulikaa na Mheshimiwa Waziri na timu yake na wakapeleka wataalam kule Hai kwenda kubaini mahitaji ya wananchi. Je, ni lini Serikali itatuletea vifaa ili wananchi waweze kuunganishiwa umeme na kurekebisha miundombinu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Saashisha amefuatilia sana umeme katika jimbo lake na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri alituma timu kwenda kufuatilia. Niombe kwamba baada ya hapa tukutane ili nipate taarifa ya hiyo Kamati na nitoe maelekezo ya kufanya kile ambacho kilibainika kinaweza kufanyika ili tatizo lake la

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

muda mrefu ambalo amekuwa ukilifuatilia liweze kutatuliwa. Naomba baada ya hapa tuweze kuwasiliana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mbunge wa Jang'ombe, litaulizwa na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman.

Na. 158

Fedha za VAT zinazokusanywa na TRA Kutoka Kwenye Miamala ya Mtandao Zanzibar

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN K.n.y. MHE. ALI HASSAN OMAR KING aliuliza: -

Je, TRA itasitisha lini kukusanya na kuzirudisha fedha za VAT ilizokusanya kutoka kwenye miamala ya mtandaoni iliyofanywa Zanzibar?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mbunge wa Jimbo la Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa pande zote mbili za Muungano zimeweka msingi wa kutoza na kukusanya VAT pale ambapo huduma inapotolewa. Kwa muktadha huo, huduma ikitolewa Tanzania Bara, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatoza VAT ya asilimia 18 kwa mujibu wa Sheria ya VAT inayotumika Tanzania Bara na huduma ikitolewa Zanzibar, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) inatoza VAT ya asilimia 15 kwa mujibu wa Sheria ya VAT inayotumika Zanzibar.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutambua sehemu ambapo huduma imetumika, Serikali za pande zote mbili za Muungano ziliunda mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama *Electronic Revenue Collection System (e-RCS)* wenye uwezo wa kutambua miamala yote inavyofanyika na hivyo kusaidia kutunza takwimu sahihi za mauzo yanayotokana na miamala ya mitandao inayofanywa na watumiaji wa kila upande. Mfumo huu unasimamiwa na kamati ya wataalam wa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo ya kampuni zote za simu hapa nchini imeunganishwa na mfumo wa Serikali wa *e-RCS* na taarifa za miamala ya mitandao hutolewa kila mwezi ikiainisha bayana huduma zilizotumika Tanzania Bara na zile zilizotumika Zanzibar. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, swali la nyongeza.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Wizara kuhusiana na swali nililouliza, nina swali moja la nyongeza. Ni kwamba kumekuwa na uvumi wa muda mrefu kwamba *VAT* inayotoka kwenye miamala ya mtandao ya simu inakusanywa na mamlaka moja tu ambayo ni ya *TRA*. Halafu *TRA* ndio wanakisia kiwango ambacho wanawapa Zanzibar. Wizara wanasemaje kwenye uvumi huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la taaluma tu katika nchi yetu kwa jamii yetu kwamba *TRA* ndio wanakusanya mapato ya pande zote mbili katika suala la miamala. *ZRB* wanakusanya kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara ni

TRA. Kwa hiyo nichukue fursa hii kuwaagiza *TRA* na *ZRB* kuendelea kutoa taaluma kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili wajue makato haya yanakatwa vipi kwa mujibu wa sheria. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 159

Kumlinda Mlaji Katika Biashara Mtandaoni

MHE. JUDITH S. KAPINGA aliuliza:-

Je, Serikali kupitia Tume ya Ushindani (*FCC*) ina mkakati gani wa kumlinda mlaji katika biashara za mtandaoni?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha biashara ya mtandaoni inalindwa, Tume ya Ushindani (*FCC*) ina Mpango mkakati wa kutekeleza jukumu la kumlinda mlaji wa biashara mtandaoni 2021/2022 - 2025/2026. Mkakati huo ni kupitia njia ya elimu kwa walaji kuhusu haki na wajibu wao na mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wakifanya biashara za mtandaoni ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa taarifa zilizotolewa kwenye mtandao kuwa ni sahihi. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, swali la nyongeza.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naishukuru Serikali kwa mujibu mazuri. Suala la ulinzi wa mlaji kwenye biashara za kimtandao hauwezi kusubiri Mpango Mkakati wa Miaka Mitano kwa sababu tayari tumechelewa na hivyo madhara makubwa yanaonekana kwa walaji pamoja na wafanyabiashara.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya utaratibu wa haraka labda kwa kuweka kanuni ili kuweza kumnufaisha mfanyabiashara huyu na mlaji katika mitandao hii ya kijamii? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Judith Kapinga Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana kuhusu biashara na hasa biashara mtandaoni. Ni kweli tuna mkakati huo lakini hatuwezi kusubiri mkakati ili tuweze kutelekeza majukumu ya kumlinda mlaji kwa sababu biashara mtandaoni ziandelea. Ndiyo maana sasa tunafanya marekebisho ya Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003 ambayo pia ina jukumu la kumlinda mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi tumeshachukua hatua zaidi, tumeanza kuhamasisha biashara mtandaoni na Waheshimiwa Wabunge watakumbuka mwaka 2021 wakati wa Maonesho ya Saba Saba tumefungua biashara mtandaoni kupitia Shirika letu la Posta; Posta hii ya *commerce* na mambo mengi yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatuwezi kusubiri mkakati, kuna jitihada nyingi zinaendelea wakati pia na hili

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

la mkakati linaendelea kufanyika ili kuhakikisha tuna uhakika wa kuwalinda walaji wanaotumia biashara mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake.

Na. 160

Ujenzi wa Barabara ya Mugakorongo – Kyerwa

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa kilomita 50 za barabara ya Mugakorongo kuanzia mpaka wa Uganda na Tanzania utaanza ili kuvutia biashara na watalii?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ya Omugakorongo – Kigarama hadi Murongo yenye urefu wa kilometa 110.1 utatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa sehemu ya barabara kutoka Murongo hadi Businde eneo la Kigarama yenye urefu wa kilometa 50. Ujenzi wa sehemu hii utaanza Murongo na pia utahusisha ujenzi wa Daraja la Murongo lililopo mpakani mwa Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza na nishukuru kwa hatua ambazo Serikali imefikia kwa ujenzi wa barabara hii. Pia naomba kujua barabara ya Murushaka kwenda mpaka Murongo, ambayo walishatangaza *tender*, wamefikia wapi, ili barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

Swali la pili; tunayo barabara inayotoka Kyerwa, Makao Makuu ya Wilaya, Nyakatuntu, Kamuli, Kitwe, Mabira mpaka inaunganisha Karagwe; nataka kujua, barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wetu na ndiyo kuna uzalishaji mkubwa, lakini imekuwa ikijengwa kwa kiwango ambacho siyo kizuri: Ni lini Serikali itaweka barabara hii yote iweze kujengwa kwa changarawe ipitike wakati wote? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Omurushaka – Nkwenda - Kyerwa hadi Murongo itaanzwa kujengwa kilometa 50 kati ya Kyerwa kuja Omurushaka kilometa 50. Utaratibu utakaotumika ni kusanifu na kujenga. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii tayari *tender* ilishatangazwa na mwisho wa kupokea *tender* ni tarehe 10 mwezi huu wa Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; nampongeza sana Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kwa ufuatiliaji. Kwenye suala hili alilouliza la pili, amekuja ofisini mara kadhaa; na tumekwambia kwamba baada ya kutoa haya maelezo, tumetoa maelekezo kwa Meneja wa

TANROAD Mkoa wa Kagera ili akaangalie barabara hiyo ili iweze kutengenezwa yote kwa kiwango cha changarawe. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kyerwa kwamba kazi hiyo itafanyika katika bajeti ya mwaka unaokuja. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Aida, nimekuona.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya Namanyere – Kirando – Kipili ni barabara ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya kukuza uchumi wa Wilaya ya Nkasi na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla. Ningependa kujua ni lini ujenzi wa barabara hii utanza kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara iliyotajwa ya Namanyere – Kirando – Kipili ambayo inakwenda ziwani ni barabara muhimu sana. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tulishafanya usanifu na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami barabara hii muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania na hasa uchumi wa wana Rukwa na Jimbo hasa la Nkasi Kaskazini. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Elibariki Kingu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa naomba kuuliza swali: Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka Mgungira – Magungumka – Ufana – Mwankalaja kwenda Kaugeri, Mlandara hadi Mwaru? Kwa maana barabara hii imejengwa madaraja kwa kipindi cha miaka 12, mpaka leo madaraja haya hayajakamilika kwa maana ya kujengewa tuta.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili *TANROADS* waweze kukamilisha ujenzi wa barabara hii?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kingu, Mbunge wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu Mheshimiwa Kingu tuweze kuonana. Kama barabara imejengwa kwa miaka 12 na haijakamilika, tuweze kuona changamoto ni nini? Nitakuomba Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuweze kukaa tuone nini cha kufanya kuikamilisha hii barabara muhimu sana kwa Wana-Singida lakini pia wananchi wa Jimbo lako. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali kwa leo umemalizika. Tunaanza na matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii. Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza kuwatangaza wao.

Wageni Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji, ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Pangani; Mheshimiwa Haji Juma Haji na Mheshimiwa Mwandambo Sali Hassan. Karibuni sana wageni wetu kutoka Pangani. (*Makofi*)

Wageni 13 wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejemi, Mbunge, ambaye Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao ni marafiki zake kutoka *Golden Fork Restaurant* ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Meneja wao, Ndugu Mohamed Said. Naona hawajapata fursa ya kuingia.

Kuna wageni sita wa Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mbunge ambao ni Balozi wa Utalii na Mkurugenzi wa Isabela

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Africa Foundation kutoka Kilolo na Arusha Mkoani Iringa wakiongozwa na Balozi wa Utalii Ndugu Isabella Mwampamba. Wako pale, Karibuni sana. (Makofi)

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Kitila Mkumbo, Mbunge, kutoka Dar es Salaam, Dkt. Richard Shukia. Naye naona hayupo.

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Yahya Mhata, Mbunge; ambaye ni Katibu Tarafa kutoka Nanyumbu Mkoani Mtwara, Ndugu Livinus Nchimbi. Karibu sana, yule kule yuko juu. (Makofi)

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Nusrat Hanje ambao ni wafanyakazi wa *Palm Village* wakiongozwa na Mmiliki wa Mradi wa Nyumba za Makazi na Biashara *Palm Village* kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Jonson Huang Mmiliki wa *Palm Village* Meneja Masoko. Karibuni sana katika Bunge letu. (Makofi)

Pia tuna wageni 170 wa Mheshimiwa David Kihenzile ambaye pia ni Rais wa *Tanzania Red Cross* ambao ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa *Tanzania Red Cross* Taifa wakiongozwa na Makamu wa Rais wa *Tanzania Red Cross*, Ndugu Lucia Pande. Karibuni sana watendaji wa *Red Cross* kutoka huko. (Makofi)

Pia tuna watendaji wa *Tanzania Red Cross* wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Felician Mutahengerwa. Karibuni sana. (Makofi)

Vile vile tuna wawakilishi kutoka Vuguvugu la *Red Cross* Duniani (*Red Cross Movement*) wakiongozwa na *Head of Cluster Juba Delegation IFRC*, Ndugu Papaa Mousa Tall. Karibuni sana (Makofi)

Pia tuna vyama rafiki duniani (*Sister National Society*) walihudhuria wakiongozwa na Katibu Mkuu *Kenya Red Cross Society* Ndugu Asha Mohamed. Karibu sana. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Pia tuna Viongozi na watumishi wastaafu wa *Tanzania Red Cross* wakiongozwa na aliyekuwa Rais wa *Tanzania Red Cross*, Ndugu Mwadini Jecha ambaye pia alikuwa Mbunge wa Jimbo la Wete Pemba 2000 hadi 2010. Karibu sana. (Makofi)

Tuna Wajumbe wa Baraza la Vijana la *Tanzania Red Cross Society* ya Taifa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Ndugu Alex Daud. Karibuni sana. (Makofi)

Pia kuna Wajumbe wa Kamati ya Uchaguzi ya *Tanzania Red Cross* wakiongozwa na Mwenyekiti Wakili Ipyana Mlilo. Karibuni sana. (Makofi)

Wageni wengine ni Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa yanayoshirikiana na *Tanzania Red Cross* wakiongozwa na *UNICEF, WFP UNHCR*. Karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Venant Daudi, ambaye ni Diwani wa Kata ya Miyenze ambaye ni Ndugu Daniel Zengo. Naona hayupo huyo.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo kutoka Mkoani Mbeya ambao ni Ndugu Edward Mhami na Ndugu Rehema Mwang'ombe. Wapo pale, karibuni sana katika Bunge letu. (Makofi)

Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu ambao ni Padre kutoka Jimbo la Katoliki la Sumbawanga, Ndugu Father Wilbroad Benedict Kazumba. Pia Ndugu Christopher Nazil Kipele kutoka Kwela na Ndugu Irene Hermes Bureta kutoka Kwela. Karibuni sana *father* kutoka huko Mbeya. (Makofi)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Kihenzile kutoka Dar es Salaam ambao ni Ndugu Cikay Richards, *Executive Director European Business Group*. Pia tuna Ndugu Gilman Kasiga *Country Manager General Electrics*. Karibuni sana. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Pia tuna wageni kumi wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambao ni vijana kutoka Jimbo la Hai wakiongozwa na Katibu Muhtasi wa Mbunge Ndugu Rose Temu. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo ya wageni wa Wabunge, pia kwa vile leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hayupo, kwa hiyo, Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika ndio yeye anakaimu nafasi hiyo ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni leo tarehe 8 Mei, 2022. *(Makofi)*

Pia tuna tangazo hapa la Mheshimiwa Shally Raymond ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania anawatangazia Wabunge wanawake *TWPG* kuwa kutakuwa na Mafunzo ya Uongozi kwa Wabunge wanawake wote yatakayotolewa katika makundi manne; kundi la kwanza ambalo tayari limepokea barua za ushiriki itanza mafunzo hayo leo tarehe 9 wameandika, Mei, 2022 mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge. Nafikiri ni tarehe 8 leo, mchana katika ukumbi Na. 231 *second floor* jengo la Utawala. Kwa hiyo, naamini wote wameelewa tangazo hili.

Katibu tuendelee.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UWEKEZAJI VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Hoja ya Serikali, Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara. Tuna majina hapa ya Waheshimiwa, nitaomba tuanze na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na baadaye

atafuata na Mheshimiwa Neema William Mgaya na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, ajiandae.

Mheshimiwa Neema William Mgaya ajiandae Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ya kuweza kusimama tena katika Bunge hili Tukufu. Napongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Viwanda pamoja na Kilimo inasisitiza katika suala zima la *agro-processing* kwa maana ya kuchakata mazao ili kuyaongezea thamani sambamba na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye tumbaku tumefanya vizuri tuna *TCC*, vile vile kwenye chai tuna viwanda mbalimbali vya kuchakata chai. Tukienda kwenye pamba, tuna asilimia 70 tunasafirisha pamba nje, hatujafanya vizuri. Nilikuwa naomba kilichotokea kwenye pamba tujitayarisha kisije kutokea kwenye zao la parachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu wa Njombe ni wazalishaji wazuri sana wa zao la parachichi pamoja na baadhi ya mikoa mingine ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, tuna uhakikia kabisa wa malighafi nyingi ya zao la parachichi. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuona namna ya kuhamasisha na kuwashawishi wawekezaji wafungue viwanda vingi sana ndani ya Tanzania ili malighafi hii ya parachichi itumike hapa kwetu, ichakatwe katika viwanda vyetu ili kuwaongezea thamani wakulima na kilimo chao kiwe na tija, sambamba na kuongeza ajira ambayo ni changamoto kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuiomba Wizara iangalie namna ya kuongeza viwanda vya chuma

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

vya msingi, kwa sababu Tanzania tuna viwanda vya msingi vya chuma viwili tu; tuna *KMTC* ambacho kipo Moshi na Mang'ula kile ambacho kipo Morogoro. Viwanda hivi vipo chini ya *NDC*, ni vya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia tuna viwanda vya nondo 15 ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Viwanda hivi vyote vina-*suffer raw material* ya chuma, na matokeo yake vinatumia vyuma chakavu katika uzalishaji. Vile vile tumeona tumekuwa na changamoto nyingi sana ya uharibifu wa miundombinu, watu kutafuta hivyo vyuma chakavu ili viweze kwenda ku-*supply* kwenye viwanda vile vya nondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliwahi kuzungumza kule Arusha na kutoa maelekezo kwamba Serikali ifanye mchakato haraka wa kumaliza mazungumzo na yule mwekezaji wa Liganga na Mchuchuma.

Naiomba Serikali tuendeleze hili zoezi la kuzungumza na huyu mwekezaji; huu mradi wa Liganga na Mchuchuma uweze kufanya kazi ili tuweze kupata viwanda vingi vya msingi vya chuma, tuweze kuzalisha vyuma vingi na tuweze kupata *raw material* nyingi ya chuma ambayo itatumika kwenye viwanda mbalimbali kama hivyo vya nondo.

Pia vitaanzishwa viwanda vingine vya kutengeneza mabati na misumari ili tusiwe na adha ya malighafi hii kwa sababu tunayo, tuitumie ili wananchi wa Mkoa wa Njombe, kule Ludewa na Tanzania kwa ujumla ili tuweze kunufaika nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Liganga na Mchuchuma tumeanza kuuzungumza tangu mwaka 2015. Hivi sasa ni takribani miaka saba. Kwa kweli naomba kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza, Serikali tufanye haya mazungumzo haraka ili tuweze...

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Neema Mgaya.

T A A R I F A

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Neema Mgaya kwamba mradi huu siyo tu kwamba tumeanza kuuzungumza toka mwaka 2015 bali pia ulikuwa ni sehemu ya miradi ya kimbakati katika Taifa letu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema unapokea hiyo taarifa?

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naipokea taarifa kwa mikono miwili kwa sababu alichokisema ni uhalisia kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi wa Liganga na Mchuchuma ukifanya kazi, nimeshazungumza mara nyingi sana ndani ya Bunge hili, tangu mwaka 2010, takribani miaka 12 nazungumza suala la Lianga na Mchuchuma. Kila Bajeti ina maana nimezungumza zaidi ya mara 20 ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna reli ya kisasa ambayo tunatengeneza. Kama mradi huu ungekuwa tayari umeshaanza kazi, ina maana tungetumia chuma kwa bei nafuu kuliko vyuma ambavyo vinaagizwa kutoka nje. Lakini nipende tu kukwambia na niiambie Serikali kwamba, wanasayansi ulimwenguni wako *busy* kuumiza kichwa kuangalia namna gani watapata nishati mbadala ya makaa ya mawe. Kumbumbuka kwenye Liganga na Mchuchuma kuna makaa ya mawe. Na kama wako *busy* kutafuta nishati mbadala ya makaa ya mawe kwa sababu tu ya kulinda mazingira ili kumaliza mambo ya *air pollution*; na inasadikika kwamba baara ya miaka 10 haya makaa ya mawe nchi nyingi hayatokwenda kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hofu yangu ni kwamba, yasije kutokea kama yale yaliyotokea kwenye mkonge.

Wakati tuko tayari kuzalisha hayo makaa ya mawe ndipo hapo nchi sasa hazihitaji tena. Soko tena halipo na yale makaa sasa yanakuwa hayana maana tena. Kwa hiyo, bado naendelea kuisisitiza, Serikali mmalize hayo mazungumzo ili tuwe ndani ya muda. Serikali itambue kwamba dunia haitusubiri, dunia haitusubiri, dunia inakwenda kasi hivyo lazima na sisi twende kasi ili tuweze kwenda sambamba na dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, lakini vilevile kumpongeza. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni msikivu, lakini vilevile ni mlezi. Tulizungumza sana hapa masuala ya *destination inspection* na *pre-arrival inspection*; na juzi kwenye moja ya mikutano yake ametoa maelekezo kwa Serikali, kwamba waangalie *system* ya *high breed* atakayejisikia kufanya ukaguzi nje ya nchi sawa, atakayejisikia kufanya ukaguzi wa gari lake ndani ya nchi sawa. Hii inadhihirisha jinsi gani Mama alivyo mlezi na jinsi gani Mama anavyotaka kila mtu afanye mambo kutokana na vile anavyojisikia bila kuvunja sheria za nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais na ninaomba hayo maelekezo Mheshimiwa Rais aliyoyatoa Wizara hii ifanyie kazi haraka na wale watakojisikia kufanya *destination inspection* wataendelea na wale ambao wanataka *pre-arrival inspection* wataendelea ili mradi tu kila mtu aweze kufanya mambo yake kwa uhuru na kuweza kuona namna gani inaleta tija kwa huduma atakayoipata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya. Tunaendelea na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na baadaye Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipa ili nami

niweze kuchangia hii Hotuba muhimu sana ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimepitia Hotuba, nimesoma hotuba yote ya Mheshimiwa Waziri ambayo ina kurasa zipatazo 201. Napenda nikiri kabisa kwamba taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri imesheheni mambo mengi muhimu sana katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimeangalia Taasisi zetu zinavyofanya kazi vizuri. Taasisi ya *CAMARTEC*, *TIRDO*, *TIMDO* na *SIDO*. Kazi nzuri waliyoifanya ya taknolojia ya kisasa ya kuandaa mashine ambazo zinaongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa ajili ya usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Hii ni kazi nzuri sana ambayo inafanywa na taasisi zetu hizi na mimi nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Ma-*CEO* wa taasisi hizo pamoja na watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kazi kubwa hapa ni kuzisaidia hizi taasisi sasa ziweze kufanya kazi vizuri zaidi. Utakuta taasisi kama hizi zinafanya kazi kubwa kama hiyo, lakini nenda kaangalie bajeti zao, utasikitika sana. Serikali itenge fedha nzuri, nyingi za kutosha kuziwezesha hizi Taasisi. Tuna vijana wetu waliobobea vizuri na ndio wanaoyafanya haya mambo makubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana wakaweza kupewa fursa ya kuweza kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu uwekezaji wa Serikali pamoja na sekta binafsi. Waheshiwa Wabunge hili suala la uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi linahitaji kuangaliwa kwa makini sana. Mikataba mingi tuliyoingia inanyonya mapato ya nchi. Mikataba mingi tuliyoingia katika uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi inanyonya uchumi wa nchi, inahamisha rasilimali za nchi na inahamisha ajira za Watanzania. Lakini vilevile katika mikataba hii mingi tunayoingia inapora ajira za Watanzania, kwa hiyo unajikuta kwamba mkataba unaingwiwa wa Watanzania hawa ambazo fedha za Watanzania zinaenda

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kulipa ajira kwa watu wengine wakati tunao vijana ambao wanaweza kufanya kazi nzuri sana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mikataba mingi ambayo tunayoingia ambayo ni *questionable* na mingine imetuletea madhara makubwa sana. Tunayo mikataba, sasa hivi *TPA* naye ameanza kutafuta mdau, ameanza kutafuta mbia. Mikataba ya namna hii; lakini ipo mikataba inayotusumbua mpaka sasa hivi ya *TRA* na *SISPA Company* ambayo nayo inahamisha fedha za Watanzania. Lakini ipo mikataba mingine tumeingia majuzi hapa ya India *Tech Mahindra* na *TANESCO* ya ziadi ya bilioni 70 kwa ajili ya kuendeleza mifumo ya *TEHAMA* wakati wataalam wa *TEHAMA* tunao hapa wa kila aina wanaoweza ku-*develop* mifumo ya *TEMAHA*.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wameandaa mifumo mizuri kama *GePG*, *POS* na hata *MaxMalipo*, mifumo mizuri tu. Leo unaenda kutafuta mfumo India kwa ajili ya kufanya nini? Sasa mikataba ya namna hii imekuwa ikituletea madhara makubwa sana. Na hivi sasa hivi nasikia *Symbion* inapigiwa chapua hapa tuilipe bilioni 356, bilioni 356 lakini inapigiwa hili chapuo wakati huo huo hatuambiwi aliyeingia mkataba huo na kutusababisha tuwe na mkataba ambao hatuwezi ku-*exit* hata kama mkataba ule unatuingizia hasara, amechukuliwa hatua gani? Tunaambiwa na chapuo hilo linapigwa bila kuambiwa kwamba huyu *Symbion* malimbikizo yake ya kodi ni shilingi ngani na anapaswa kutulipa shilingi ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, linapigwa hilo chapuo hatuambiwi ukaguzi gani uliofanyika juu ya mambo yaliyojificha nyuma ya pazia hili. Wabunge tukataeni mikataba ya namna hii lakini tukataeni hata kulipa hizi fedha. Uchunguzi ufanyike, ukaguzi wa kina ufanyike kilicho jificha nyuma ya *Symbion* tuweze kuyajua yote mazagazaga yaliyopo na tuweze kuzijua haki zetu zilizopo katika hilo eneo. Lakini mikataba yote ambayo tunaitambulisha kwamba ni mikataba mibovu itishwe hapa Bungeni tuweze kuifuta.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili suala la mfumuko wa bei. Suala la mfumuko wa bei. Ni kweli imeelezwa hapa kwamba mfumuko wa bei umesababishwa na UVIKO 19 pamoja na vita vya Urusi na *Ukraine*, tumeelezwa hapa. Ni kweli sababu hizi zinachangia mfumuko wa bei, lakini zipo sababu zingine ambazo zimechangiwa na ukosefu wa uadilifu wa viongozi wetu na watendaji wetu. Ziko sababu zilizosababishwa na uzembe na usimamizi dhaifu wa maeneo mbalimbali ambao tunaufanya sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema na kuliambia Bunge lako hili ni kwamba mfumuko wa bei huu unaoendelea hivi sasa umesababishwa na umetengenezwa na tumeutengeneza sisi wenyewe tuliomo humu ndani. Mateso haya ya mfumuko wa bei ambayo wanayapata wananchi sasa hivi tumeyatengeneza hapa kwa kukosekana kwa uadilifu, kwa kukosekana kwa usimamizi makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la upangaji holela wa bei. Upangaji holela wa bei sisi wote tunashuhudia hapa, bidhaa zote zimepanda bei, kila siku zinatangazwa bidhaa kupanda bei. Lakini ukweli ni kwamba pamoja na sababu zingine, sababu ya upangaji holela wa bei, mtu anaamua tu kupandisha bei hili suala limekuwa likitrudisha nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri hapa ametueleza kwamba kuna upandaji holela wa bei lakini tunachoshangaa ni kwamba kama kuna upandaji holela wa bei, na yeye Waziri anajua na anayo mamlaka yake ya *FCC* inayosimamia ushindani, na Sheria ya Ushindani Namba Nane ya Mwaka 2003, hawa watu wanaopandisha bei kiholela kwa nini hawajachukuliwa hatua? Kwa nini hawajachukuliwa hatua? Waziri anawajua waagizaji wa mafuta nje ya nchi, anawajua waagizaji wa ngano nje ya nchi, anawajua wazalishaji wa ndani na amefanya tathmini na akagundua watu wamepandisha bei kiholela. Hao waliopandisha bei kiholela kwa nini hawajarudishwa kwenye mstari ili wananchi waweze kupata bei nafuu? Waziri kwa nini anawaogopa hawa? Au

anataka kutuambia kwamba watu hawa wana nguvu zaidi kuliko Serikali? Au Waziri anaubia nao? Na kuwaacha Watanzania waendeleo kuteseka na mfumuko huu mkubwa wa bei wa kuamuliwa na watu waliokaa na kukubaliana tu tupandishe bei? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la uhaba wa nishati ya umeme. Kuhusu suala la uhaba wa nishati ya umeme, Kamati imetueleza hapa imesema ilipotembelea viwanda viwili ikaenda kugundua kwamba kuna viwanda umeme ulikuwa unakatika mara 10 ndani ya masaa manne. Ni maneno ya Kamati siyo maneno ya Mpina. Umeme ulikuwa unakatika zaidi ya mara 10 ndani ya masaa manne. Pale unategemea kuna uzalishaji gani? Uzalishaji viwandani unashuka na kama uzalishaji viwandani ukishuka wafanyabiashara wataamua kupandisha bei, kwasababu uzalishaji wao utakauwa umeshuka, ili waweze kufidia gharama ya uzalishaji na kupata faida, na ndiyo lazima upate mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

MWENYEKITI: Haya malizia

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni mafuta. Mafuta, Mbunge mwenzetu hapa Mheshimiwa Hamis Tabasam, Mbunge wa Sengerema alitueleza kuna wizi mkubwa unaofanywa kwenye *Petroleum Bulk Procurement Agency* kuna wizi mkubwa unafanyika kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi hoja ya wizi unaofanyika kule kwenye *agency* ya kununua mafuta tulitegemea ingeweza kuwekewa ukaguzi wa haraka, *CAG* na *PCCB* wakavamia wakafanya ukaguzi na kuujua ukweli kama Watanzania wamepandishiwa bei na mafisadi wachache na wezi wachache tukaujua ukweli lakini sasa hivi hoja inaondolewa kwenye wezi waliofanya wizi inapelekwa kwenye tozo ambazo hizi tunapata shughuli za maendeleo nyingi kutokana na hizo tozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi *seriousness* yetu iko wapi? Watanzania wanalia, wanapandishiwa bei za mafuta, watu wanatangazwa kufanya njama za manunuzi, wanafanya wizi kwenye manunuzi, wanapandisha bei makusudi, tunaletewa taarifa hapa Bungeni ukaguzi haufanyiki na uchunguzi haufanyiki. Ni lazima mambo haya tuyakatae na lazima tuwahurumie Watanzania.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mpina. Tunaendelea na Mheshimiwa Cosato David Chumi. Baadaye atafuatia Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi; na napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitazungumza mambo mengi, mimi najielekeza kwenye jambo moja tu, ambalo linagusa viwanda pamoja na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Neema na mimi kwa miaka kadhaa sasa nimekuwa nikishauri kuhusiana na suala la sukari; na wakati wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilisema kuhusiana na mafuta ya kula; na juzi Mheshimiwa Injiniya Ezra amesema, Mheshimiwa Kingu na Wabunge wengine wamesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama taifa lazima tufike mahali kuna mambo tuyakatae, na kama Bunge lazima mahali tufike kuna mambo tuyakatae. Sasa tunayakataa mambo gani? Na tunayakataaje? Kati ya mambo ambayo tunatakiwa tuyakatae moja wapo ni hili la kuagiza bidhaa kutoka nje ambazo tunaweza kama taifa kuzalisha hapa hapa nchini. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukawa tunaagiza mafuta ya kula, tunaagiza ngano, tunaagiza sukari. Mjumbe mmoja alisema hapa. Kwa mfano tunategemea mafuta ya kula kutoka Malaysia kwa asilimia kubwa, *what if* siku ikitokezea soko kubwa liko Marekani wakaelekeza mafuta yao yote kwenda Marekani, na sisi tutafanya nini kama taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yako mambo lazima kama taifa tuyakatae, kwa sababu haiwezekani kama Taifa sisi ni kuagiza tu, ni kuagiza tu, ni kuagiza tu vitu ambavyo tunaweza kuzalisha hapa nchini. Hii mifumuko ya bei, ugumu wa maisha tunaosema ni kwa sababu pia takriban kila kitu tunaagiza. Yaani ukiangalia sisi kama taifa kitu ambacho ambacho hatuagizi ni hewa tu ya Mwenyezi Mungu ambayo ametugaia lakini *a lot of things* sisi ni kuagiza! ni kuagiza! ni kuagiza!. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri jambo hili tulikatae kama taifa. Tutakataaje? Mwaka 2019 tarehe 15 mimi baada ya kuchangia, pamoja na mchango wangu wa maandishi niliandika barua kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Kilimo, Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Fedha. Niliandika barua kuwaambia namna ambavyo kama taifa tunaweza tukaondokana na shida ya kuagiza sukari kila mwaka. sasa kwa nini niliandika barua hiyo kwa Mawaziri hawa? Ni kwa sababu sukari ni biashara lakini ni viwanda; lakini kabla hujapata sukari lazima mtu wa kilimo awe amehusika katika kulima miwa.

Pia ili aweze kulima miwa lazima Waziri wa Fedha kwa namna moja ahusike katika masaula mazima ya *financing*. Yuko Waziri mmoja sitamtaja alinjibu na haikuwa lazima ile barua wanijibu, hapana, ulikuwa ni ushauri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama taifa, wenzetu Brazili na India wamefanikiwaje katika sukari? Wametumia *small scale industries*. Kwamba unakuwa na maeneo ambayo yako *suitable* kulima miwa, lakini pia gharama zake si kubwa katika kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nashauri tuwekeze kwenye *small and medium scale sugar plantations*? Kwanza kiwanda hakihitaji eneo kubwa, kina hitaji kama heka tano tu, na pia unahitaji kama heka 3,000 za kuzalisha miwa. Lakini pia ukishazalisha miwa hiyo heka 3,000 ambayo niliwaandikia watu wa Kilimo na TAMISEMI; unaweza kushirikiana na Halmashauri za maeneo husika zenyewe zikatoa ardhi, Wizara ya Fedha wana-*finance* kupitia hata Benki ya Kilimo na uwekezaji wake hauzidi dola kati ya milioni 3.5 hadi milioni 5. Maana yake hapo unazungumzia bilioni nane. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hata ukiwa na wale wakulima wa nje (*out growers*) inakuwa ni rahisi kuwapa *extension services*. Lakini pia ukijenga viwanda hivi vidogo vidogo hata gharama za usafirishaji wa miwa kutoka shamba kwenda kwenye hiyo *factory* hauwi mkubwa kama ilivyo sasa. Tunazungumza mradi wa Mkulazi, huu nadhani ni mwaka wa sita. Mradi wa Dola milioni 150 lakini sisi hapa tukiwa na Dola milioni 100 kwa miaka miwili hatutaagiza sukari nje na tutauza sukari nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yapo. Kuna Manyara, Mfilisi, Kibelege Ifakara, Luembe, Wami, Kasulu na Lufiji. Kwa sababu nchi yetu imejaliwa hali tofauti tofauti. Kwa hiyo, mimi nashauri sana Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ikae kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Rais ameunda kikosi kazi chini ya Profesa Mkandala kwa ajili ya kuzungumza na kujadili namna gani mustakabali wa kuendesha siasa zetu katika hali iliyo njema na bora. Mheshimiwa Waziri...

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Cosato. Mheshimiwa Kingu.

T A A R I F A

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kumpa mchangiaji kaka yangu Mheshimiwa Cosato Chumi kwamba mikakati ya kuwekeza katika viwanda vya *TCD* ndogo vyenye uwezo wa kuzalisha kuanzia tani 100 na kuendelea aliyekuwa Mkurugenzi wa *NSSF* wakati huo ambaye sasa ni Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Uwekezaji na Viwanda alishakuja na mipango mikakati kwa ajili ya kujenga viwanda vidogo lakini mipango hiyo masikini ya Mungu sijui imepotelea wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa taarifa hii anachokisema Mheshimiwa Cosato Chumi tunauwezo wa kujenga viwanda vya *TCD* ndogo ndogo tukaeupukana na uagizaji wa sukari na kuliokoa Taifa letu katika kutumia fedha za gigeni kwa ajili ya uagizaji wa sukari. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cosato Chumi unaipokea hiyo taarifa?

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na Mheshimiwa Kingu ninaamini ni miongoni mwa walionielewa ninacho kimaanisha. Naamini ataungana na mimi ninaposema kama taifa kuna mambo tukatae. Kwa muundo huo wa kuwa na viwanda vidogo vidogo ambavyo tunaweza kushirikisha, kama nilivyosema, Halmashauri zikatoa ardhi, Benki ya Kilimo ikatoa mitaji, Wizara ya Kilimo ikasaidia katika namna ya kuhakikisha kwamba tunakuza hiyo miwa. Mimi ndugu zangu nimekaa Kilombero, miwa ukipanda ni miezi 12 unaanza kuvuna na baada ya hapo kila baada ya miezi sita utavuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaposema tukatae ndiyo mambo kama haya kwamba anasema hapa Mheshimiwa Kingu. Bahati nzuri Profesa mko nae huko sasa aliyekuwa *NSSF* ndiye Katibu Mkuu; na ndiyo maana nasema Mheshimiwa Waziri pamoja na ile timu yako unaweza ukawa na kitu kinaitwa *kitchen cabinet*...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia muda wangu kidogo. *Kitchen cabinet* ni nini?

MWENYEKITI: Malizia kidogo.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na timu yako unaweza ukawa na timu ya wataalam kutoka *SUA*. Kama tumeunda kikosi kazi kwa ajili ya mambo ya siasa, kwa nini tusiunde kikosi kazi kwa ajili ya mambo ya uchumi? Ili tukatae mambo ya kuagiza, ukachukua wataalam kutoka *SUA*, ukachukua wataalam kutoka *UDSM* pale, kutoka Mzumbe, kutoka hapa Chuo cha Mipango wakasaidia nao kama *kitchen cabinet*. Simaanishi kwamba wataalam ulionao hawana uwezo, hapana, ili wakushauri ipasavyo ili kusudi dhana ya kwamba tukatae, tukatae, tukatae baadhi ya mambo izeze kuthibitika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nakushukuru. Nilisema siku moja, katika baadhi ya maeneo *along the high way* naomba Serikai itusaidie. Watu kama wa Mafinga, Mikumi, Makambako, Mombo – Korogwe na kwingineko turuhusiwe kufanya biashara masaa 24. Tujiongezee kipato na Halmshauri zipate kipato, kwa sababu sheria *as it is now* mwisho kufanya biashara ni saa nne. Lakini hata dunia zingine watu wanafanya shughuli saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono na Mungu atubariki. Mungu abairiki taifa letu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasunga baadaye Mheshimiwa Stella ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nianze kwanza kuipongeza Wizara, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu kwa ujumla kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakifanya, pia niipongeze Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa taarifa yao nzuri ambayo wamefanya uchambuzi wa kina nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika taarifa zote zinaonyesha kwamba mchango wa ukuaji wa sekta ya viwanda Tanzania umefika asilimia 8.9 sasa katika mazingira tuliyonayo asilimia 8.9 ni ukuaji bado huko chini hauendani na hali halisi ya changamoto tulizonazo na mahitaji tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma nchi yetu ilibahatika, tuliweza kujenga viwanda vya aina zote, toka tumepata uhuru tulijenga karibu viwanda vya aina zote. Tulikuwa na viwanda kwanza ni sera ya Chama cha Mapinduzi sasa hivi, Chama cha Mapinduzi kimetoa sera ni moja ya malengo kwamba lazima tujenge viwanda na viwanda ukiviangalia ndio vitatoa suluhu ya matatizo yote tuliyonayo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huko nyuma tulikuwa na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao. Baba wa Taifa alijenga viwanda karibu vyote vilikuwepo! Tulikuwa na viwanda vya kuchakata nyama, viwanda vya kuongeza thamani ya nyama, viwanda vya ngozi vilikuwepo na mazao mbalimbali ya Ngozi, viwanda vya misitu na mbao vilikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mashine viwanda vya *tools* za uzalishaji vilikuwepo vililijengwa, mpaka tulipofika mwaka 1974, 1975 karibu viwanda vyote vilikuwepo, viwanda vya nguo vilikuwepo, viwanda vya korosho vilikuwepo, viwanda vya mafuta vilikuwepo, viwanda vya kila kitu vilikuwepo vyote. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabati yalikuwepo, misumari yaani hatukukosa kiwanda cha aina yoyote. Swali ambalo tunatakiwa tujiulize ni nini kilitokea viwanda hivyo vyote vikafa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijua pale tulifeli nini ndipo tutakuwa na mkakati ambao unafaa katika kujenga viwanda kwa sasa, bila kuelewa tulikotoka hatuwezi kujenga viwanda! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara, nimesoma taarifa nafurahi wana mikakati mizuri lakini nataka hasa wanasaidie ni upi mkakati wa Wizara wa kuongeza viwanda na ajira hapa nchini ambao kweli huo mkakati tukiuangalia kama Bunge tutaridhika kwamba nchi hii itatoka hapa tulipo tutafika mahali ambapo tunataka kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la Pili ni upi mkakati wa Wizara wa kuongeza tija na thamani ya bidhaa zetu! Bidhaa zetu ni duni haziwezi kuimiri ushindani katika soko la dunia. Sasa mkakati wetu tunaouweka ni upi ili tupate bidhaa zitakazoweza kushindana katika soko la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la Tatu ni upi mkakati wa Wizara wa kuongeza biashara ili tupate fedha nyingi za kigeni kwa sababu biashara ndio zinazoleta fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la Nne, ni upi mkakati wa Wizara wa kuja na Mfuko wa Kujenga Viwanda? Hapa tutaimba! Tutaimba! hivi mfuko wa kujenga viwanda hivyo huko wapi? Je tutajenga viwanda hivyo kwa kuzungumza kwa kuhamasisha tu, au lazima tutengeneze mazingira ambapo watu wanaweza wakapata mtaji, wanaweza wakapata fedha na tunaweza tukajenga viwanda eneo tukatengeneza kabisa tukajenga baadhi ya viwanda, tukawavutia wawekezaji, wao waje na mitaji, waje na mashine lakini tuwe tumeshajenga miundombinu yote pale! Upi hasa mkakati ambao tumeuweka, hapo unafikiri ni muhimu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni upi mkakati ambao tumejipanga kama wizara kuhakikisha kwamba tunatumia fursa zilizopo. sasa hivi, *DRC* wanajiunga Afrika Mashariki. *DRC* ni soko kubwa, tumejipangaje sasa kuhakikisha hii *DRC* inapokuja tunaenda kufanya biashara tunatumia fursa tuliyonayo tuweze kuchukua lile soko la *DRC*. Hili ni suala nafikiri ni la msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni upi mkakati wa Wizara wa kuongeza ubunifu. Tunayo *SIDO*, naelewa nimesoma yote lakini inatosheleza kuja na ubunifu tukawa wabunifu wa kutosha? Kwa hiyo nilikuwa nadhani tufike mahali sasa kama nchi tuangalie sekta ya viwanda na biashara ndiyo sekta mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuchumi tunasema uzalishaji una maeneo matatu, kuna viwanda, biashara, huduma, hizo zote ni biashara. Sasa basi kwenye viwanda tuna viwanda mama, lakini tuna viwanda kwanza vile vya kuchakata vya kutafuta malighafi yaani tunaita *extractives industries* ambayo tuna kilimo, mifugo, uvuvi, madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo vyote ni kwa ajili ya kutafuta malighafi, halafu tunakuja na viwanda sasa vya kuongeza thamani hizo malighafi ambayo tunayo, sasa hivi unajenga kiwanda cha nguo Tanzania unataka upate pamba, pamba haijazalisha kwa hiyo ina maana kama hatuta-*link* viwanda na biashara na kilimo hatutaweza kufanikiwa, hatuwezi kufika. Kama hatuta-*link* viwanda na biashara na madini hatuwezi kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuta-*link* viwanda na ufugaji na uvuvi hatutaweza kufanikiwa, kwa hiyo utakuta kwamba Wizara ya Viwanda ni mama lakini lazima ishirikiane na hizi Wizara, mkakati uwe mmoja, hapo tutaweza kufikia ile ajenda tunayoitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakwenda pale kwenye biashara, biashara inaweza ikawa ndani inaweza ikawa biashara ya nje, inaweza ikawa ni *wholesale* inaweza

ikawa *retail*, zile biashara zote ni sehemu za ajira tukipanua biashara vijana wetu wote watafanya kazi, watakuwa na ajira hatutakuwa na tatizo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni huduma, kuna huduma za elimu, kuna huduma za afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa malizia sentensi yako.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka kusema ni kwamba kwenye huduma huku ndiyo tunatakiwa tutumia hiyo nafasi. Kwa mfano, sasa hivi tumejenga vyuo vya elimu vingi sana hapa nchini viko zaidi ya 30, vile vyuo tunatakiwa tuweke mazingira vidahili wanafunzi kutoka nchi za nje ili watulettee fedha za kigeni na nchi itapata hela nyingi sana. Ninaamini kwa kufanya hivyo tutaweza kupata mchango mkubwa na uchumi wetu utakua kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kuunga mkono hoja, nawapongeza lakini nataka waje na mikakati madhubuti ambayo Bunge hili litaamini na litaweza kuyapitisha kwamba sasa tunaenda kujenga uchumi wa viwanda, tunaenda kufanya biashara, tunaenda kuongeza uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Stella Saimoni Fiyao, Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Usonge Hamad Juma ajiandae. *Ok* tunaendelea na Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwa uchache kwa habari ya hoja iliyopo mbele yetu inayohusu uwekezaji viwanda na biashara, mimi

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ningependa kuchangia eneo moja tu pengine mawili hasa upande wa stakabadhi za ghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipata fursa ya kutembelea Mikoa ya Kusini kwa maana ya Mtwara, Ruvuma pamoja na Lindi kujionea ni namna gani mfumo wa stakabadhi za ghala unafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tulijiridhisha vya kutosha pasipo shaka kwamba mfumo huu ni mzuri na unaweza kuisaidia nchi kuweza kufanya shughuli za uratibu unaotokana na shughuli hasa za mazao. Tulivyoangalia ule mfumo ule kwanza unawasaidia sana wananchi kuweza kupata soko la Pamoja, wanavyojiunga kwenye vikundi inasaidia kutafuta soko kwa haraka lakini kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulichoona kwamba unasaidia utunzaji wa mazao katika maeneo yenye viwango vizuri kwenye maghara na hivyo inasaidia mazao kutokuharibika, kwa sababu ukiangalia katika maeneo mbalimbali namna ambavyo tunatunza mazao yetu imekuwa ikisababisha mazao yetu kupata sumu kuvu. Kwa hiyo, kwa mfumo huo wa kutumia stakabadhi za ghala inasaidia sana mazao yetu kutunzwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho tuliona kwamba huu mfumo unalinda wazalishaji wadogowadogo, kinachofanyika ni kwamba wenye fedha wafanyabiashara wa mazao ni rahisi kwenda kuokotaokota mazao kwa wakulima wadogowadogo mwenye magunia mawili, matatu, kwa hiyo unakuta kwamba inawanyonya kwenye bei, lakini kama wakiweza kuuza kwa pamoja inawasaidia kupata bei nzuri. Kwa hiyo ni mfumo mzuri ambao mimi nimeona unafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninachokiona kwamba kwenye huu mfumo kumekuwa kuna malalamiko mengi kwamba wananchi mazao yao wakati mwingine hayapimwi katika vipimo rasmi lakini kwa kupitia mfumo huu inasaidia sana wananchi waweze kupima mazao yao katika vipimo

ambavyo ni rasmi na vinaweza kuwasaidia wao kuweza kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani tulishaweza kusikia Mzee Mangula alikuwa analima viazi akawa analalamika kwamba wananunua kwa lumbesa lakini kwenye mfumo huu sasa inasaidia kwa sababu tunakuwa na mizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilichokiona kingine ni kwamba wananchi wanaweza kupata elimu ya pamoja, kama watu wamekaa katika vikundi ni rahisi Maafisa Ugani, Maafisa Kilimo kuja kuweza kuwaelimisha kwa hiyo ni jamba zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliona jambo lingine zuri katika mfumo huu kwamba pembejeo zinaweza kununuliwa katika maeneo ya uhakika kuliko tunavyoona sasa mtaani kuna viuatilifu na pembejeo feki, lakini kwa kupitia mfumo huu wa stakabadhi za ghala ni rahisi sana kuweza kusaidia watu kupata pembejeo katika maduka ambayo ni rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nililiona, kwa sababu katika safari ile pia tulikuwa na taasisi za fedha, kwa hiyo watu wakikaa katika mfumo huu wa stakabadhi za ghala inasaidia sana kuwa *accessible* kirahisi na hizi benki zinaweza kuwakopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni changamoto zipi ambazo tuliziona, tulivyotembelea pale wananchi wengi walitoa shuhuda wao kwamba maisha yao yameboreka, wamejenga nyumba wanasomesha Watoto, lakini changamoto kubwa ambayo tuliiona ni kwamba kumekuwa na ucheleweshaji wa malipo ya fedha, kwa hiyo unakuta kwamba wanapeleka bidhaa leo lakini anaweza akalipwa baada ya miezi mitatu, hiyo inawachelewesha wakati mwingine kufanya mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tuliliona uaminifu kwa wale watunza maghala, unakuta

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kwamba umeleta mzigo wako labda wa korosho, wale wasimamizi wanasema pengine korosho zako zilikuwa na unyaufu wa asilimia fulani, kwa hiyo ni changamoto nyingine. Lingine ambalo nililionga ni kwamba kuna changamoto ya maghala ambayo hayana viwango, hizo ni changamoto tatu ambazo tuliziona. Sasa ni nini mapendekezo yangu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho niliona ni kwamba mapendekezo ambayo mimi ninayatoa hivi Vyama Vikuu viwe na mtaji angalau wa kulipa asilimia fulani wakati mkulima anavyoleta mazao yake ili kuweza kumudu yale mahitaji madogomadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninashauri kwamba hivi vyama viwe na uwezo wa kununua angalau pembejeo za kuanzia ili wanachama wao waweze kupata pembejeo kwa wakati angalau zile za kuanzia. Pia benki ziangalie kutoa mikopo kwa wakati, maana hili pia lilikuwa ni lalamiko ambalo nililionga wananchi wanasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutengeneze maghala yenye viwango, kwa sababu unaweza ukaona kwenye kutunza kwa mfano mbaazi haziwezi kutunzwa katika mazingira fulani kwa muda mrefu yanaweza kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine vyama viwe na vipimo vya kuangalia unyevu kwenye mazao hiyo ni mapendekezo ambayo naona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakala wa vipimo wahakikishe mara kwa mara wanapita kukagua ile mizani kuona kwamba inapima vizuri kwa sababu ile mizani imekuwa na tabia ya kuchezele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu pia iendelee kutolewa hasa kwa viongozi na sisi wanasiasa, maana inaonekana kwamba huu mfumo bado hatujaelewa, wakati mwingine pengine *interest* zetu, wakati mwingine pengine atuelewi tu mfumo, mimi nilivyoona kwanza utawasaidia wananchi pamoja na Serikali kupata zile tozo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwa na uhakika kwamba kama nchi fulani inataka mazao ya kiasi fulani ni rahisi kuweza kujua kwamba Songea tuna dengu kiasi fulani tuna mbaazi kiasi fulani ni rahisi kufanya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwe na vyama vichache vyenye nguvu badala ya kuwa na vyama utitiri ambao wakati mwingine ni utapeli. Tukiwa na vyama vichache vyenye nguvu vinaweza kufanya mambo yake vizuri. Tumeona vyama kule Mbinga tumekwenda, kule Namtumbo wanajenga sasa hivi kiwanda chao cha kutengeneza vifungashio ni kwa sababu ni viwanda ambavyo vimeimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba kwenye Benki angalau ziendelee kuwa chini kwa sababu hii pia ni changamoto kubwa ambayo tuliiona. Mfumo wa stakabadhi za ghala pia napendekeza uende nchi nzima nina fahamu kupokea au *adoption* mara nyingi ni shida sana hapa nchini, hata wakati tunaanza LUKU walikuwa wanakataa lakini sasa ndio imekuwa kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naona katika mapendekezo minada iwe ya wazi, yaani minada siyo tu mtu anakuja na karatasi kwenye boksi mnada ufanyike kwa uwazi kama inavyofanyika ukienda wakati mwingine sokoni watu wanauza mia tano, mia sita, mnada ukifanyika wazi ni rahisi watu kupandisha bei. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Usonge Hamad Juma baadaye Mheshimiwa Daniel Sillo utajiandaa.

MHE. JUMA USONGE HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuimarisha biashara zetu ndani ya nchi, pia niwapongeze sana Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Katibu Mkuu kwa uandaaji mzuri wa taarifa hii na kuwasilisha hapa leo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki nizungumze sana lakini zaidi nataka nijikite kwenye zao kuu la mwani. Zao kuu la mwani ni zao la kibiashara ambalo sisi kama Taifa tunategemea soko kubwa sana kupitia wenzetu wa Zanzibar pia kupeleka nje ya nchi zao hili la mwani. Pia kuna asilimia kadhaa ambayo tayari inabakia hapa kama malighafi kwa ajili ya utengenezaji na uchakataji wa sabuni, viyoyozi, *cosmetic product* pamoja na masuala ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la mwani ni kama mazao mengine kwa mfano karafuu zao la korosho, ufuta na mazao mengine tofauti tofauti lakini ni jambo la kushangaza kuona kwamba zao la mwani halijapewa kipaumbele Zaidi. Naweza nikasema kwamba zao hili linaonekana kama labda wakulima wa mwani ni watu ambao wako kwenye hali duni ya kipato chao ambacho wanachokiendesha kwa ajili ya kulivuna zao hili la mwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba zao hili la mwani kupitia Wizara hii bado halijapewa kipaumbele zaidi mbali na jitihada kubwa ambazo zinazofanywa kupitia na wenzetu wa *TANTRADE* lakini pia kuna wenzetu wa *TIRDO* wamefanya *intervention* kubwa na hivi juzi tu mwezi wa tatu tulienda pale *TIRDO* Dar es salaam, tukaona kuna *sample* zaidi ya 99 wamezichukuwa kwa ajili kufanyia utafiti, lengo hasa na madhumuni ni kuona kwamba hili zao la mwani linakuwa na soko lakini pia lina toa *product* ambazo tayari zitatumika ndani ya nchi lakini pia zitatumika ndani ya nchi

lakini pia zitatumika nje ya nchi, hivyo nawapongeza sana *TIRDO*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo pia niwapongeze sana *TIRDO* na kuwapa salamu za akina Mama kule Kisiwani Pemba kwa kuwajengea majokofu kwa kiingereza tunaita *seaweed dryer* majokofu ambayo *especial* kwa ajili ya ukaushiaji wa ule mwani ili mwani ukishakaushwa ukitoka pale utatoka mzuri lakini hautakuwa na vimelea vyovyote ambavyo vinaweza vikaathiri kwa hiyo niwapongeze sana ndugu zangu wa *TIRDO* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze sana ndugu zangu wa *TANTRADE* kwa kuona kwamba kuna umuhimu mkubwa sana ndugu zetu hawa akina Mama ambao ndiyo asilimia 90 wanajishuhulisha na zao hili la mwani wanawapatia fedha pia wanawapa elimu. Wamefanya kazi kubwa ingawa bajeti yao tunafahamu ni ndogo lakini wanafanya kazi kubwa mno kwa ajili ya kuwasaidia hawa akina Mama, ndiyo maana leo hii ukipita kwenye maonyesho ya Biashara kama utaenda Zanzibar ama utakuja Tanzania Bara bidhaa ambazo zinaonekana kushamiri kwa wingi kwenye maonyesho ya biashara ni bidhaa ambazo zinatokana na hizi za mwani, hivyo ninawapongeza sana ndugu zangu wa *TIRDO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji nguvu kazi kubwa kwa ajili ya kulinusuru zao hili la mwani. Zao hili la mwani tukilisafirisha nje tunaingiza pesa nyingi za kigeni na tukizibakisha hapa tunaingiza fedha nyingi za Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zao hili la mwani limetengeneza fursa za ajira hususani kwa kinamama ambao wako kando kando ya bahari, tunayo mikoa i zaidi ya minne kwa Tanzania Bara, lakini kwa Zanzibar kuna mikoa mingi sana ambayo tayari inashamiri kwenye zao hili la mwani, lakini jitihada za Serikali bado zinaonekana ndogo kwa ajili ya kutafuta masoko. Zao hili la mwani miaka ya nyuma lilikuwa na thamani kubwa, katika matajiri ambao tayari

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

utakaowazungumza kando kando ya bahari, basi ni wakulima wa mwani, lakini sasa hivi zao letu hili la mwani limesharaulika, limesharaulika kupita maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara iliingalie tena zao hili la mwani. Zao hili la mwani linanusuru asilimia 90 akinamama ambao tayari wako kando kando za bahari, hawana shughuli nyingine yoyote ya kufanya isipokuwa kulima zao hili la mwani. Kama Serikali kuna umuhimu mkubwa sana tukakaa kwa pamoja kuangalia masoko ya nje na ya ndani ili mradi zao hili la mwani kuliongezea thamani ili akinamama wale wasikate tamaa na kuweza kumudu familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kupitia zao hili la mwani ili sasa lizidi kupata soko, pia tuweze kupata fedha za kigeni. Jambo la kwanza; tuna makampuni machache ambayo tayari yananunua mwani. Kwa hiyo, Serikali lazima tuangalie makampuni haya kunaonekana kuna urasimu wa hali ya juu, wanajipangia bei wanayoitaka wao wenyewe, hali ya kuwa kwamba ukiangalia kwenye soko la kidunia mwani una *value* kubwa lakini pia una fedha ndefu, lakini makampuni ambayo tayari yamepata *accreditation* kwa ajili ya kununua huu mwani ni makampuni machache. Hivyo naiomba sana Serikali iangalie namna ya kuruhusu makampuni mengine yote duniani yaje kununua mwani Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakinunua mwani hapa nchini kwetu naamini kwa asilimia 100 mwani utapanda bei na wananchi wetu ambao tayari wako hali duni za kiuchumi, basi wanaweza wakauza huu mwani kwa bei iliyokuwa ni nzuri. Kwa sasa hivi makampuni mawili kununua mwani, ni sawasawa na kufanya biashara ya *monopoly*, si sahihi kwa nchi yetu ya Tanzania wakati *value of money* ni kubwa, lakini mwani unanunuliwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niwaombe sana ndugu zetu wa *TANTRADE* tunao ma-*expert*, tunao wataalam, tuwatumie hawa kwa ajili ya kushuka chini kwa wakulima

wetu kwenda kuwapa elimu namna gani ya kuchakata huu mwani ilimradi kwamba tupate bidhaa bidhaa ambazo tayari tutaziuza kwa thamani iliyokuwa nzuri ili mradi kwamba sasa wakulima wetu waweze kuuza huu mwani, wapate fedha na kuendesha familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu; elimu ya ujasiriamali ya hali ya juu nayo pia itolewe, bado wakulima wetu elimu yao ni ndogo sana kwa ajili ya uchakataji wa huu wa mwani ili mradi kutoa bidhaa ambayo tayari itakayouzika. Kwa hiyo naomba sana watumie taaluma ya hali ya juu, watafute watu wa *marketing*, kisha warudi kwa wakulima wetu, bidhaa ambazo tayari wanazalisha kule mitaani, basi wazifanyie *marketing*, wazi *brand*. Pia zipate *national identity*, zijulikane hizi bidhaa zinatoka nchini Tanzania. Tukifanya hivyo zao letu hili la mwani litapata *value* kama mazao mengine kama vile yalivyo mazao ya korosho, karafuu na mazao mengine yalivyokuwepo duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, kuna mfumo wa stakabadhi ghalani ambao umejikita zaidi kwa mazao haya ya biashara. Zao la mwani pia ni zao la biashara, hivyo naomba sana mfumo wa stakabadhi ghalani nao utumike kwa ajili ya kununua mwani, lakini mwani ukishanunuliwa, lazima uwekwe stoo ili mradi wanunuaji lazima waje kununua mwani kwenye stakabadhi ghalani. Tukifanya hivyo, naamini kwa asilimia 100 zao hili la mwani litakuwa kubwa, lakini pia wakulima wetu watashukuru sana kupitia haya mambo ambayo tumeyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana na naunga mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Usonge. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Sillo na Mheshimiwa Josephat Gwajima ajiandae.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara yetu hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Kwanza

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupanua diplomasia ya Kimataifa ya kiuchumi ambako sasa itafungua fursa kubwa nyingi sana za uwekezaji hapa nchini. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri wetu wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, dada yangu Mheshimiwa Ashatu pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi zile wanazozifanya pamoja na hotuba nzuri aliyowasilisha katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika maeneo machache la kwanza ni mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchi (*easy of doing business*). Kwenye ukurasa wa 26 mpaka 27 wa hotuba hii, ameelezea ufanyaji wa biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Benki ya Dunia ya Mwaka 2018 inasema Tanzania ilikuwa nchi ya 141 kati ya nchi 190; lakini nchi ya jirani ya Kenya ilikuwa 56 kati ya nchi hizo 190; Uganda ilikuwa 116; Rwanda ilikuwa ya 38. Mwaka 2019 Tanzania ni nchi ya 141 kati 190 na Kenya ya 56, Uganda 116 na Rwanda 38. Nchi yetu katika *region* hii ndiyo iko chini kabisa urahisi waufanyaji biashara hapa nchini. Kwa hiyo niombe sana Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara iitoe nchi yetu katika..

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Abbas Tarimba.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, anayozungumza Mheshimiwa Sillo ni mambo mazito sana, ni mambo muhimu sana na ukiangalia maandiko mengi ya Serikali yanahubiri *private sector* kwa maana ya taasisi binafsi au sekta binafsi kwamba ndiyo *engineer* ya *growth*, kila mahali Serikali inazungumzia hivyo. Vile vile ukiangalia *Tanzania Private Sector Engagement Fact Sheet* inatuambia

kwamba *private* sector yenyewe mchango wake ni asilimia 90 ya ajira hapa Tanzania, lakini vile vile ni asilimia 60 ya uwekezaji na zaidi ya asilimia 80 ya kodi za Serikali. Hivyo analolizungumza ni suala zito ambalo naliunga mkono, naomba nimpe taarifa katika mchango wake. Ahsate sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Daniel Sillo taarifa hiyo.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ya Mheshimiwa Tarimba, mjumbe makini kabisa wa Kamati ya Bajeti naipokea kwa mikono yote miwili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwarobaini wa tatizo hili nini? Mwarobaini wa suala hili ni ukamilishaji wa *Blueprint for Regulatory Authority* – Mpango Maalum wa Kuboresha Ufanyaji wa Biashara hapa Nchini. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hili jambo la *Blueprint* limeanza muda mrefu, naomba likamilike. Zipo taasisi za Serikali zinafanya ama shughuli zinazofanana, lakini mwekezaji au mfanyabiashara anaingia kwenye taasisi nyingi za Serikali. Naamini kabisa kama huu mpango utakamilika basi itarahisisha sana ufanyaji biashara hapa nchini. Tunalia kila siku kwamba tupanue wigo wa walipakodi, tunapokuwa tunawafukuza hawa wafanyabiashara hatuwezi kukuza wigo wa walipakodi hapa nchini na kwa maana hiyo Serikali inapoteza mapato mengi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarijia kupata ajira kwa Watanzania Ilani ya Uchaguzi ya 2025 inasema tuajiri Watanzania milioni nane. Bila kuwezesha Sekta Binafsi hatuwezi kufikia lengo hilo, kwa hiyo niombe sana Wizara iboresha mazingira ya wafanyabiashara hapa nchini ili nchi yetu itoke kwenye *rating* hii ya nchi iende kwenye hatua ya juu kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la kuelekeza; nielekeze kwenye mifumo, ukienda kwenye taasisi zetu unakuta kuna *OSHA*, kuna *TBS*, kuna *TMDA* waweke mifumo inayosomana ili mwekezaji au mfanyabiashara akienda ofisi

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

moja akilipa basi iende moja kwa moja kwenye zile *sector* zingine kuliko kumsumbua mfanyabiashara aingie jengo hili, aingine jengo lile, tunajikwamisha wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la uwekezaji. Hapa naipongeza Serikali imechukua hatua mbalimbali katika mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Tunapenda Kituo chetu cha Uwekezaji (*TIC*) pamoja na *EPZ* kiwe ni *one stop shop* kwamba akiingia mfanyabiashara pale, mambo yake yote yanakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye *EPZA* tuna *TRA* pale, tunataka mifumo isomane mtu wa *TRA* pale awe na maamuzi, akishaona mfuko umehakikiwa pale ukienda bandarini unasafiri kwenda nje ya nchi bila shaka biashara inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwenye eneo la *TIC* pia tuweke wataalam wa Serikali wenye maamuzi. Inapoteza muda mwingi sana unaweka watu ambao hawana maamuzi, *document* zinafika pale zinabebwa kwenda makao tena tunapoteza muda mwingi sana wa wafanyabiashara. Kwa hiyo niombe sana wawepo watu watoa maamuzi wa Serikali katika maeneo haya ambayo tunayasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana, tumeletewa wawekezaji wengi, kwa hiyo, niombe sana Wizara ijielekeze katika kuhakikisha kwamba tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika juhudi hizi za kuweka wawekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine ya wawekezaji, yapo mashamba makubwa ya wawekezaji hapa nchini, lakini yana migogoro na wananchi, mashamba hayaendelezwi, watu wamewekeza, wanachukua robo ya shamba, lingine sijui wanakopea, kwa hiyo, wananchi wetu hawapati maeneo ya kufanya shughuli zao za uchumi kama kilimo, ufugaji na kadhalika. Niombe sana Wizara ijielekeze kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukiwa na migogoro mwekezaji hatawekeza. Kwa hiyo hata Serikali inakosa mapato iliyotarajia, lakini wananchi wetu wanakosa kufanya shughuli zao za uchumi, lakini Serikali pia inakosa mapato ambayo ingeyapata. Kwa hiyo niombe sana Waziri wetu msikivu kabisa, dada yangu Mheshimiwa Ashatu ajielekeze kabisa ili wananchi wetu waendeleo na shughuli zao za kiuchumi kwa manufaa makubwa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, kule Halmashauri ya Babati kuna mashamba makubwa kwenye Kata za Kiru, Magugu, Magara na Kisangaju lakini migogoro mitupu. Napongeza Serikali kuna ziara za Waziri wamefanya kazi kubwa, lakini bado migogoro ipo. Naiomba Serikali iweze kujipanga vizuri kumaliza migogoro hii ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Sillo. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephat Gwajima na Mheshimiwa Condester Sichelwe ajiandae.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa hizi dakika chache za kuchangia katika hoja ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda pamoja na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anafanya kazi kwa bidii kuwapigania Watanzania na kulipigania Taifa letu, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru ndugu zangu Mawaziri kwa namna wanavyofanya kazi kwa bidii kumsaidia Mheshimiwa Rais ili kutimiza ndogo ya wananchi. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Nataka nijikite sana kwenye suala la Liganga na Mchuchuma. Liganga na Mchuchuma imekuwa hoja ya muda mrefu sana pengine watu hawajui Liganga ni nini? Unaposema Liganga ni mlima wa chuma, ni mlima wa *iron ore*, si chuma ya kuingia chini kuchimba ni mlima wa chuma na uposema Mchuchuma ni mlima mwingine wa makaa ya mawe ambavyo hivi viwili mlima wa chuma pamoja na mlima wa makaa ya mawe ya kuiyeyushia hiyo chuma yamewekwa na Mwenyezi Mungu kwenye eneo moja ili kazi iwe rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana, ni vizuri pia kugundua kwamba, uzinduzi wa Liganga umefanyika 1860 karne ya 18, hiki chuma cha Liganga kikagunduliwa hapa Tanzania na uvumbuzi wa hii Mchuchuma kwa maana ya makaa ya mawe ni 1898. Ina maana Mwalimu Nyerere akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa anajua, Mzee Mwinyi alikuwa anajua, Mzee Mkapa alikuwa anajua, Mzee Jakaya Kikwete alikuwa anajua, Mzee Magufuli alikuwa anajua na Mama yetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan pia anajua kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kujiuliza ni kwa nini pamoja na hiki chuma kugunduliwa muda mrefu karne ya 18, lakini hatujachimba na mahitaji ya chuma ni makubwa hapa Tanzania, ni kwa nini hasa? Kwenye kuzungumza kwangu kwa dakika chache nitawagusa baadhi ya watu siyo kwa ubaya bali kwa lengo la kusaidia nchi yetu. Nipo hapa Bungeni kwa lengo la kusaidia nchi na si vinginevyo. Kwa hiyo katika kuzungumza nikimgusa mtu nisifahamike nimemgusa kwa ubaya bali nimemgusa kwa maslahi mapana ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nitoe takwimu kidogo ya uingizaji wa chuma Tanzania. Kwa mfano, mwaka 2018 tumeingiza chuma cha thamani ya dola milioni 401.2 hapa Tanzania, tumenunua sisi. Mwaka 2019 tumeingiza chuma ya thamani ya dola milioni 491.9 hapa Tanzania. Mwaka 2020 tumeingiza vyuma vya thamani ya dola ya

milioni 423.4 hapa kwetu Tanzania. Mwaka 2021 tumeingiza chuma ya dola ya thamani ya milioni 7.8. Mwaka 2022 tumeingiza chuma ya thamani ya dola milioni 235.7 hapa kwetu. Kwa hiyo kwa miaka hii mitano tumelipa fedha ya kigeni kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi kwa ajili ya chuma, dola bilioni 2.2 kutokea hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu yeyote mwenye akili na anayejua kuzitumia, jambo hili haliwezi kuruhusu kufanyika kama chuma ipo hapa Tanzania. Sasa unihurusu niongee machache kidogo, ni kwa nini sasa hili jambo halijafanyika? Hebu nikupe mawazo, kwamba, tumeanza na reli, ujenzi wa reli *standard gauge a good idea very good idea* na si kinyume na hapo. Kwenye ujenzi wa reli, *component* kubwa inayotumika ni chuma, sasa ilikuwaje tukaanza kujenga reli kwa kuagiza chuma kutoka nje ya nchi badala ya kutengeneza chuma chetu kwa kuchimba ndiyo tukaanza na reli, ilikuwaje? Ni kitu gani kinatokea mpaka *priority* ya kwanza inakuwa ya mwisho na ya mwisho inakuwa ya kwanza. Kinachosumbua ni kukosa Maono ya Taifa, Mipango ya Taifa na Dira ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simlaumu mtu yoyote. Nataka sasa unisikilize vizuri, kwa mfano, kama kungekuwa na maono ya Taifa juu ya viwanda maana yake kungekuwepo maono ya muda mrefu yanayoelezea juu ya chuma kilichopo Tanzania. Kwa hiyo, tusingekuwa tumeanza na reli, tungekuwa tulianza na fedha ya kuchimba chuma ili chuma chetu kije kitengeneze reli zetu, tungeokoa mabilioni ya shilingi tunayoyasema hapa. Nchi yetu inahitaji maono au *agenda* ya Taifa ya pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikiliza, jambo hili linaonekana kwamba *its nonsense, its chasing wind* lakini sikiliza niwaambie nchi nyingi zilizoendelea zina maono ya nchi zao ya muda mrefu. Hakuna nchi duniani iliyoendelea kwa muda wa miaka mitano au kwa muda wa miaka kumi. Nchi huwa zinaendelea kwa kuweka maono ya miaka mingi, unaiona nchi kwa mbali, wanafunzi wataiona nchi kwa mbali, wasomi wataiona nchi yao kwa mbali. Tukifanikiwa kuiona

nchi kwa mbali tunaweza kuisukuma Tanzania kuipelekea mahala ambapo inatakiwa kuwa.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, Kingu hapa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Kingu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa msemaji kaka yangu Askofu Gwajima, kuonesha kwamba pia kuna mahali tuliteleza, sisi tumefuta hata tume hiyo ya kutengeneza mipango ya muda mrefu wa nchi. Leo tunapozungumza kwenye Taifa letu hatuna kitu kinaitwa Tume ya Mipango ambayo ndiyo wanatengeneza *plans* za nchi za miaka hamsini na kwenda mbele, *we don't have* Tume ya Mipango.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gwajima taarifa hiyo.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Kingu ana taarifa nyingine za namna hiyo aendelee kunipa, naendelea kuzikubali. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kinachosumbua sana ni mipango ya muda mrefu. Tungekuwa na mpango wa muda mrefu wa hii Mchuchuma ni aibu. Nikupe mfano; kuna *Paris Agreement on the use of coal* ambayo imeweka ukomo wa kutumia makaa ya mawe na ukomo huo ni 2030. Hebu jaribu kuwaza tangu makaa ya mawe ya kwetu yamevumbuliwa karne ya 18 mpaka yanataka kufikia ukomo hatujayatumia bado, *what can you call this*, hiki kitu unaweza kukiitaje? Kwamba Mungu amewawekea mlima wa chuma, halafu amewawekea moto wa kuyeyusha hiyo chuma palepale, hamwezi kuitumia mpaka unafika wakati umefika ukomo wa kutumia 2030, hatujaitumia, jambo hili hatutakiwi kuliruhusu hata kwa dakika moja, hata kwa sekunde moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kinatuleta mpaka hapa, kukosa maono. Naomba viongozi wetu waliopo Mawaziri,

Manaibu Waziri waliopo Serikalini pamoja na mama yetu mwema, mama anayewapigania Watanzania, mama Samia Suluhu Hassan, zawadi peke yake tunayoweza kuipa nchi hii kwa sasa hivi ni maono ya nchi ili watu waweze kuiona nchi kwa mbali nawaweze kupanga mipango yao sawasawa na maono ya nchi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gwajima subiri kidogo, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitambue mchango mzuri anaoutoa Mheshimiwa Mbunge na Mtumishi wa Mungu Askofu Gwajima; lakini nilitaka niweke tu kumbukumbu sawa kwamba Taifa letu mara zote limekuwa na mipango ya muda mrefu na mara zote tangu uhuru limeongozwa na viongozi wenye maono. Kumbukumbu mbili hizo; moja, tumekuwa na mipango ya muda mrefu na ndiyo maana tulikuwa na Dira ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya 2025 ilitungwa wakati wa Mkapa na miaka yote hii ikamegwa kwa miaka mitano mitano; na utekelezaji wake ukianza na dira ya kwanza, na ya pili na hata tunayoenda kumalizia, ilikuwa na mtiririko ambayo ukienda kwenye *headings* zake zimeongelea mpaka na hizi habari za viwanda, habari hizi zote ambazo tunaongelea za kukuza uchumi na hata sasa tunapomaliza 2025 tayari tumeshaanza kuandika dira nyingine ambayo kimsingi kwenye mijadala tunaangalia ama tuandike kwa utaratibu wa miaka 20, 20 au tuandikie tuoanisha na Dira ya Afrika iende 2063.

Kwa hiyo, mipango ya muda mrefu ipo kwenye nchi yetu na hii ndiyo inayozaa utekelezaji huu wote ambao tunaoufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maono, nchi yetu isingezongwa kwa maono tusingekuwa hivi tulivyo leo, imeongozwa kwa maono ndiyo maana tumefika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambieni ndugu zangu Watanzania, tusipende kujidharau, nchi zote majirani; *SADC* na Afrika Mashariki wanapenda maono ya Tanzania. *Actually*, wao wanaiona Tanzania ndiyo mfano. Kwa hiyo, tusijidharau. Ila tunapopeana fursa za kujirekebisha zaidi, turekebishe ili twende kwa kasi zaidi, lakini siyo kwamba nchi haijawahi kuwa na viongozi wenye maono na kwamba nchi haijawahi kuwa na mipango. Nchi nyingi tu hata mipango wanayotekeleza mingine wame-*copy* kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona tu niyaseme hayo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri naamini umeeleweka. Mheshimiwa Askofu Gwajima, taarifa ya Mheshimiwa Waziri hiyo.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia, kwa mfano sasa hivi, Mheshimiwa Rais tayari ameshaweka kwenye *pipe line* utekelezaji wa hii miradi mikubwa, yote hii tunaenda kuitekeleza. Tunatekeleza Liganga, tunatekeleza *LNG*; hivi tunavyoongea, inaenda kutekelezwa siku siyo nyingi. Yote hayo ni maono na ni utekelezaji wa mipango...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, nafikiri umeeleweka, taarifa hiyo Mheshimiwa Gwajima.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu kaka yangu Waziri wa Fedha na Mipango kwa staha kubwa kwa sababu yeye ni mwakilishi wa Serikali. Amethibitisha tu kwamba Mpango uliyopo ni mpaka 2025 na wanajiandaa kuandika Mpango mwingine. Amenithibitishia kwamba hatuna mpango wa miaka 50, hatuna mpango wa miaka 100. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa kunisaidia kwa hilo. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikae kwenye hoja yangu. Ninachosema mimi, sidharau kilichofanyika na Serikali. Ninachosema, tukiwa na mipango ya miaka 50 au miaka 100, wanafunzi wakaiona nchi yetu kwa mbali; kwa mfano tukiwa na mipango ya muda mrefu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa malizia, muda ulikuwa umeenda, lakini malizia dakika moja.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona nikichangia muda unapungua, itabidi niombe Kanuni muda unapungua inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu kwamba kwa ufupi tukiwa na mipango ya muda mrefu juu ya viwanda, wanafunzi wanaosoma shule wataiona nchi yao kwa mbali na watajua wasome nini kwa sababu wanaweza kuyasoma maono ya Taifa. Hicho ndicho ninachosema. *I am not attacking anybody, I am trying to improve* kwamba mahali tulipo ni pazuri, lakini tukiwa na mipango. Tungekuwa na mipango juu ya hili, tungekuwa tumeanza na kuchimba chuma chetu ili chuma chetu kitumike kwenye reli, hii fedha *2.2 billion dollars* iliyoenda nje kununua chuma ingekuwa imebaki hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Condester Sicalwe.

MHE. CONDESTER M. SICALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Ni Condester Sicalwe. Ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na kuishukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Momba, nashukuru sana kwa miradi yote ambayo tulipewa pesa ndani ya Jimbo la Momba. Yawezekana hatujafika pale mahali tunapotaka, lakini tunasema asiyeweza kushukuru kwa kidogo, hawezi kushukuru hata akipewa kikubwa. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania; pamoja na changamoto yote ya mfumuko wa bei tunayoipitia, wanaendelea kupambana kuhakikisha wanaijenga nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka leo hoja yangu nielekeze katika kuishauri Serikali na kuiomba. Nimesoma vizuri sana Taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara, lakini kuna kipengele ambacho natamani kuona Serikali inawasaidia wananchi wa chini kabisa; mwanachi yule aliyeko kijijini ambaye hajui hata kusoma na kuandika, anaweza akatumia uwezo wake na maarifa yake ambayo Mwenyezi Mungu amemsadia katika kuzalisha viwanda vidogo vidogo na kufanya biashara ndogo ndogo ambazo zinawasadia kulea watoto wao na kuwasomesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapotupelekea Vituo vya Afya na Zahanati, wanafanya hizo biashara ndogo ili waweze kupata fedha ya kununua dawa kwenye vituo vyetu. Pamoja na kwamba Serikali imetoa elimu bila malipo, kuna kununua daftari, *uniform* za watoto na michango mingine elekezi ambayo imewekwa kwenye shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapotoa mchango huu, nataka nijielekeze kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano ambao unaanzia mwaka 2021/2022 mpaka 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Tafsihi yake ni kwamba tunapotaka kujenga viwanda, vifanane na maendeleo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea *Local Industry* na *Consumers Industry*; na hapa nataka kuongelea pombe za kienyeji. Pombe za kienyeji kwenye makabila mbalimbali na mikoa mbalimbali; kila makabila wana pombe zao za kienyeji. Kuna pombe ya ulanzi inatengenezwa kule Iringa, kuna mbege kule Kilimanjaro, dengelua, ntulu kule Singida kwa kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, pombe ya

mnazi kwenye mikoa huko ya Pwani; pia kuna kindi, kimpumu na pombe nyingine ambazo Serikali imezizuia, mfano gongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Wizara ya Viwanda na Biashara, kwanza kabisa iiunde bodi kama ambavyo Wizara ya Kilimo imefanya, imeunda Bodi ya *CPB* ambayo inasimamia mazao ya nafaka na mazao yote mchanganyiko. Mfano sijui mpunga, mahindi, dengu na mazao yote. Wizara ya Kilimo imeunda bodi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, pombe hizi ambazo naweza nikasema Serikali haijazipa kipaumbele na imezidharau, wakati mwingine wanasema matapatapu. Ukionekana wewe unakunywa kindi, kimpumu au gongo, hujielewi, huna akili kabisa. Ila ukionekana unakunywa bia ambazo watu wa *TBL* wanatengeneza, unaonekana ni wa kisasa. Hata ukienda kwenye Balozi zetu huko kuna ile inaitwa *Cartas*, wanawatengea kabisa fungu kununua zile pombe za bei ghali ya shilingi 300,000 , ya shilingi 400,000 , lakini zote ukizionja ladha yake haina tofauti na gongo. Tunajuliza, swali ni kwamba, ni sababu hizi zina jina la Kizungu na gongo ina jina la Kibantu?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, bodi hii itakapoundwa, inatasaidia kwenda kupima kiwango ambacho gongo inapotengenezwa. Je, mlishawahi kupima mkaona ni nini watu wa *TBS* wanaweza wakatusaidia kutoa makali ambayo yapo kwenye gongo yafanane na konyagi na pombe nyingine hizo ambazo mnazona ni za kifahari ambazo matajiri wanakunywa, lakini wote wakinywa wanalewa?

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kupitia Bunge hili Tukufu, pombe hizi za kienyeji ambazo tumezidharau, wapo wafanyabiashara wakubwa na mashuhuri ambao bibi zao, mama zao, shangazi zao, wamewasomesha kupitia hizi pombe za kienyeji. Wapo Wabunge humu ndani ya Bunge lako hili Tukufu ambao ni wasomi na ni maarufu na tunawajua

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

na nianaamini hata kaka yangu Mwigulu huko kwao atakuwa amesomeshwa na pombe hizi za kienyeji.

Mheshimiwa Spika, pia huko nyuma mimi nilishawahi kusoma *profile* moja ya Kiongozi mkubwa sana hapa nchini ambaye alihojiwa na vyombo vya Kimataifa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na yupo hapa kwenye Bunge hili Tukufu akasema kwamba amesomeshwa na bibi yake kwa kutumia pombe za kienyeji. Yupo mahali hapa, nione kama hawezi kuthibitisha.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Watanzania na Wabunge mliyopo humu ndani, ni nani hapa aniambie hawezi kutamani mtoto wake asome awe Profesa kama Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo? Ni nani aniambie? (*Makofi/Kicheko*)

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Condester, taarifa.

TAARIFA

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa na Askofu hapa; kwa hiyo, kidogo ni changamoto. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa mchangiaji kwamba kule kwetu Kijiji ninachotoka kinaitwa Mgela, pale tumejenga mpaka Kilabu cha Pombe na tumekijenga vizuri na ni *source* kubwa ya mapato. Kwa hiyo, ni mchango wake mzuri sana. Ni kweli mimi nimesoma kwa pombe, kwa hiyo, mchango wake ni mzuri sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Condester.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake. Yupo Mbunge mwingine hapa, mama yangu anaitwa Mheshimiwa Tendega, naye

amesoma mpaka Chuo Kikuu kupata digrii yake kwa wazazi wake kupika pombe za kienyeji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa msingi kwa Serikali, miradi mikubwa yote kama *SGR*, sijui Bwawa la Mwalim Nyerere, tunaipenda sana. Ndani ya Jimbo langu tuna miradi mikubwa mitatu ambayo ina-*worth* mabillioni ya pesa, lakini miradi hii mpaka sasa hivi tunavyoongea ina zaidi ya miaka mitano haijatekelezeka. Swali la kujiuliza: Je, wananchi hawa tunapoendelea kusubiri hii miradi mikubwa itekelezeka hawaumwi? Hawasomeshi Watoto? Hawaishi? Wakiumwa wanatibiwa na nini? Wanafanya shughuli hizi hizi, pombe za kienyeji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofanya ziara na Naibu Waziri wa Utawala ambao wanasimamia *TASAF*, iko chini yao, alipojaribu kuwatembelea wamama ndani ya Jimbo la Momba; wamama ambao wanafanya vizuri kwenye *TASAF* wakipewa pesa, ni wale ambao wanatengeneza pombe za kienyeji.

Sasa mimi najiuliza, sisi kila siku hatuwezi kuthamini vilivyo vyetu. Kama ambavyo wamechangia Wabunge wengine hapa, sisi kila kitu ni ku-*import*, kila kitu ni ku-*import*; jamani hata pombe tu, hatuwezi kuwasaidia hawa watu ambao wanatengeneza ulanzi kule Iringa wapate ithibati?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuipa ithibati kimpumu, kinde ambazo zinatengenezwa kule Momba? Hatuwezi kuwasaidia wamama na wabibi wa Kitanzania tupate wasomi wengi kama akina Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo? Mpaka sasa hizi tunaendelea kuongea suala la Liganga na Mchuchuma, tutasubiri miaka 50...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MHE. ESTHER N. MATIKO: ...lakini pombe hizi wananchi wanakula, wanaishi, wanavaa, wanasomesha watoto wao. Mimi nawajua vijana wengi wa Kitanzania wanaendesha V8 huko, mama zao wamewasomesha kwa kupitia pombe za kienyeji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Waziri wa Viwanda na Biashara atakaposimama hapa, aseme kuhusiana na pombe za kienyeji siyo kushika tu shilingi yako, nitaikwapua shilingi yako. Nitataka aseme neno kuhusiana na pombe za kienyeji wanakujaje? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sichalwe, nilikuongezea dakika mbili.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia hizo dakika mbili. Nimefanya utafiti wangu kuonyesha kwamba kuna soko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Muda wake umeisha Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sichalwe, mwache akupe taarifa kwa ufupi.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitamalizia hoja yangu. *Okay.*

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Condester; mchango anaoutoa ni mzuri na *valid* kwa Watanzania wote. Kwa hiyo, napenda kumpa taarifa kwamba kuna kipindi

Watanzania ambao wanazalisha mafuta kwa njia ambazo zilikuwa hazijarasimishwa, walikamatwa na Jeshi la Polisi na Waziri wa Kilimo akatoa tamko akasema Watanzania hao wasikamatwe, badala yake wasaidiwe ili waweze kujikwamua zaidi na kuweza kupimwa na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mchango wake huu, ni kweli na dhahiri unasaidia Watanzania wengi. Hata wakitaka kuchukua takwimu hapa, ni zaidi ya asilimia 70. Basi Serikali ichukue hawa Watanzania wanaofanya biashara ya pombe zilizotajwa hapa, wasikamatwe na kupelekwa Magerezani, na badala yake wawezeshwe kuhakikisha kwamba inakuwa ni pombe ya kiwango na inangia kwenye *market*. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Condester.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa taarifa, nimepokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutaka kuonesha kuthibitisha, wenzetu nchi za jirani wana-*support* watu ambao wanatengeneza pombe za kawaida. Nimekuja na *sample* za pombe za bei rahisi kabisa hapa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa muda wake umemalizika, namwachia amalizie.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pombe kama hii inauzwa sijui shilingi 1,000 inatoka Malawi; pombe kama hii inauzwa sijui shilingi 8,000 inatoka Zambia...

(Hapa Mhe. Condester M. Sichalwe Alionesha chupa za pombe mbalimbali)

MBUNGE FULANI: Ni gongo hiyo!

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Zote hizi ni gongo, Shilingi 1,500 na zimeingia nchini kinyume na utaratibu. Hizi ni gongo zimepewa majina ya kizungu, *owners* kutoka Zambia; sijui lulars whisky kutoka Zambia; sijui Jambo gin, sijui *K-Vant*, sijui icelandan... (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sichalwe umeeleweka sana, nashukuru kwa mchango wako. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Namalizia na mchangiaji kwa upande wa Bunge, Mheshimiwa Shigongo, Makamu Mwenyekiti wa Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Shigongo. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa rafiki yangu Mheshimiwa Condester umenichukua kidogo, nikawa nimepoteza kidogo *direction*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuishukuru sana Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Makamu, Katibu Mkuu na ninawashukuru pia Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu Tanzania miaka miwili iliyopita tulisherekea tukashangilia kwa pamoja kupanda mpaka uchumi wa kati. *GDP* ya Taifa ilikua, *per capital income* ikaongezeka, na hivyo tukasherekea kwamba nchi yetu inakwenda vizuri, lakini ninavyozungumza na wewe hivi sasa, nchi yetu imerudi ilipokuwa. Pato la Taifa (*per capital income*) la Mtanzania imeshuka mpaka 976. Ina maana tumeporomoka chini kwa sababu yoyote ile; iwe ni sababu ya *COVID* au ya kitu chochote, lakini ukweli ni kwamba tumeporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu kama Wabunge, kama Watanzania ni kuhakikisha tunafanya kazi kwa nguvu tena kurudi tulipokuwa na kwenda mbele zaidi. Hili

litawezekana kwa jambo moja kubwa, *Agriculture*. Kilimo peke yake; kilimo cha nchi yetu ndiyo kitatupeleka tena tulipokuwa na hata kuwa na *per capital income* ya dola 4,000 au 5,000 tuweze kukua zaidi. Kilimo peke yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Kamati ya Viwanda na Biashara leo, sizungumzii Wizara ya Kilimo. Sasa hoja yangu iko wapi? Watanzania wanalima sana, lakini kinachowasumbua ni soko la mazao yao. Watanzania siyo masikini, ila wanakosa soko la mazao yao. Hili lazima nilizungumze kwa utaratibu na nieleweke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha nchi hii kinachangia asilimia 27 ya pato la Taifa. Maana yake ni kwamba kama tukiamua kulima kwa nguvu kubwa zaidi, tutaweza kuchangia hata asimilia 50 ya pato la Taifa. Ardhi tunayo, ardhi yetu ni *square kilometer* 940 *arable land*. Inayoweza kulimika ni *square kilometer* 345,000 hivi, lakini nchi kama Malawi inatuzidi kwenye pato la Taifa katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuzungumza kitu kimoja, Wizara ya Viwanda na Biashara ina Kitengo kinachoshughulika na masoko, na Kitengo hiki ni *TANTRADE*, wapo hapa wananisikia. Nimeshawahi kukutana nao mpaka ofisini kwangu nimeongea nao, nimewaleza *what to do?* Tufanye nini kama Taifa ili tuweze kusaidia kilimo chetu? Mheshimiwa Bashe analima sana, lakini hauzi mazao. Kazi ya Bashe ni kulima, na kazi ya kuuza mazao ni ya dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji. (Makofi)

Mheshimiwa Menyekiti, sasa *TANTRADE* hawa ninaowaongelea, nitumie neno hili; linaweza kuwa siyo zuri lakini naomba wanivumilie, wako *ICU*. *TANTRADE* wako *ICU*, hawana pesa za kutafuta masoko, wanawezaje kushindana na Kenya? Wanawezaje kushindana na Malawi? Hawana fedha halafu tunategemea Mheshimiwa Bashe alime, halafu atafute masoko. Watatafutaje masoko hawa? Hawana uwezo, hawana *technology*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokizungumza na nieleweke, kama tumedhamiria kurudi tulipokuwa kiuchumi, pato la Taifa liongezeke, *per capita income* iongezeke, ni lazima kuanzia sasa tuamue kuwekeza. Hatuwezi kupeleka wanajeshi wetu vitani bila silaha. Tuna tabia ya kupeleka wapiganaji halafu hatuwapi silaha. Unategemeaje wewe Mheshimiwa Bashe unalima, halafu kesho unataka uongeze pato la Taifa, halafu hutafuti masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtafuta masoko hana fedha anahangaika, kazi yake imebadilika kuwa kuandaa sabasaba kila mwaka; kazi ya *TanTrade* siyo kuandaa sabasaba, kazi ya *TanTrade* ni kutafuta masoko yenye mazao ya nchi yetu. (*Makofi*)

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Shigongo.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge Eric Shigongo kwamba amesema tuliingia uchumi wa kati lakini tena tumerudi tulipokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumtaarifu ni kwamba, kilichotuingiza uchumi wa kati tumekiacha ndiyo maana tumerudi tulipokuwa; hii ni kwa sababu ya kukosa dira ya taifa na maono ya taifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shigongo taarifa hiyo unaipokea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, naweka sawa hiyo.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo au nikae kwanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ulikuwa unasemaje.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti nataka niweke kumbukumbu sawa; kwamba hatujarudi tulipokuwa; hii naomba isikike vizuri sana. Tulitoka uchumi wa chini, tukaenda uchumi wa kati wa chini, hatujawahi kurudi uchumi wa chini. Nchi yetu bado iko *middle income*. Tunachokiongelea ni ukuaji peke yake. Yaani hizi *terminology* za kiuchumi ni vizuri sana kuzisogelea kwa utaratibu. Kuta tofauti sana kati ya *level of income* ya nchi na *growth rate*.

Kwa hiyo sasa hivi ambacho kimeathiriwa na *COVID* pamoja na vitu vingine vyote ni *growth rate* tu; na yenyewe ni *trend* zinazobadilika kama mfumuko unavyobadilika. Kwa hiyo kilichobadilika tulishafika asilimia 7 tukashuka mpaka asilimia nne ya ukuaji wa uchumi ile ya *annual growth rate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa hivi tumeshapanda kutoka hiyo asilimia nne tumeshakwenda asilimia 4.9; na takwimu hizi zinapokamilika za 2021 *likely* ukichukua *quoters* ambazo zimekwishajumlishwa, ukijumlisha wastani unakwenda kwenye 5; na 2022 wastani unaotarajiwa ni 5.2....

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:...kwa maana hiyo; hata wenzetu wa Benki ya Dunia juzi walisema huenda tukaenda 5.5. Na kwa sasa hivi ambavyo tunategemea kuwekeza pakubwa kwenye bajeti inayokuja kwenye sekta za uzalishaji tunategemea tutakwenda kwenye hiyo saba. Kwa hiyo, hatuongelei *level of income* tunaongelea *growth rate*.

MWENYEKITI: Umeeleweka ahsante Mheshimiwa Waziri; Mheshimiwa Shigongo karibu umalizie.

MHE. ESTHRE N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Huku.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee; na kama siendelei naomba muda wangu uhifadhi kwenye friji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shigongo naomba usubiri kuhusu utaratibu. Msiwe mnahata nafasi mimi naangalia sauti yako huku kumbe upo huku. Mheshimiwa kuhusu utaratibu?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu ulikuwa unakwenda kwa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Ulikuwa unatafakari sauti kabla hujaniona; lakini nimesimama kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida ambayo inakwenda kinyume na Kanuni zetu. Kwanza tunatakiwa tunapotoa taarifa isizidi dakika mbili; lakini Mheshimiwa Mwigulu Nchemba akisimama anahutubia zaidi ya dakika mbili, kinyume kabisa na taratibu; na hii imeshawahi kutolewa angalizo na Mheshimiwa Spika hapa baada ya kuombewa mwongozo. Tunaomba tu-*observe* Kanuni zetu, kama Waziri umeshindwa kuvumilia uje kujibu mwishoni basi ukisimama ujihakikishe unaji-*confine* ndani ya dakika mbili unatoa ule taarifa yako watu wanaendelea siyo unanza kuhutubia kabla ya muda wenyewe husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Easter tumepokea kuhusu huo utaratibu na naamini wenyewe wamesikia na kwa vile imeshatolewa mwongozo basi tunaomba wajirekebishe. Mheshimiwa Shigongo naomba uridhie.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi kama mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi, mwaminifu, Mbunge wa Chama cha Mapinduzi siyo vizuri sana kupisha na Waziri wangu wa Fedha. Lakini *document* hapa inanionesha hivi; *qualification of a country to become middle income is per capital income of USD133,000 to USD 445,000*; yaani *qualification* ya nchi yoyote kuwa uchumi wa kati ni pato lake la mtu mmoja *per capital* kufikia dola 1036 sisi tulifikia Dola 1080; tuka-*qualify* kuwa uchumi wa Kati. Lakini hivi sasa *record* zilizopo hapa

zinaonesha uchumi wetu sisi sasa hivi pato la mtu mmoja *per capital* imefikia 976. Ndiyo maana nasema tumerudi kwa sababu *per capital income* imeshuka.

Mheshimia Mwenyekiti, nchi hii imepiga hatua kubwa sana, kazi kubwa sana imefanyika; tulikotoka na hapa tulipo ni pazuri sana; lakini hoja yangu ilikuwa ni kwamba kurudi nyuma kwetu hapa sisi siyo sababu, kazi yetu ni kuwaomba Wabunge na watanzania tufanye kazi kwa juhudi kubwa turudi tulipokuwa. Sasa itawezekanaje hili; hili linawezekana kwa kilimo; na kilimo tuanzie sokoni, kwanza tutafute soko ndipo tuje tuwaambie wakulima walime nini, na hiyo kazi ni *Tantrade*. Kwahiyu Tamtrade *TanTrade* wawezeshwe, wapate fedha, watafute masoko halafu wakulima waambiwe walime nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wangu wa Buchosa wwalliambiwa walime maparachichi, lakini hivi sasa yanawaozea. Sasa watu wanalima miwa inawaozea, *TanTrade* wapewe fedha, *TanTrade* wapo *ICU*, tuwatoe *ICU* kwa kuwapa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia, na kumbukumbu zikae sawasawa; kama tukiwa-*impower* watafuta masoko wetu; na wananchi wetu wakalima uchumi wanchi hii utakua, pato la taifa litaongezeka na watanzania watakuwa na fedha. Kwa hayo, ninayosema nakuona unagusa kengele bila shaka unataka kunisimamisha; ahsante naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shigongo.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kinachoishia Aprili, 2022 Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya viwanda na pia kuna mwelekeo mzuri wa kuboresha mazingira ya biashara (*blueprint*). Pia kwa kusimamia vizuri diplomasia ya uchumi, imejenga imani kubwa kwa wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuwekeza kwenye maeneo muhimu ya uchumi wetu. Katika kipindi cha mwaka mmoja na miezi minne, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, imetekeleza miradi mingi ya viwanda na pia kuboresha mazingira ya biashara (*blueprint*) kwa kuondoa tozo, ada na kodi ambazo zimekuwa kikwazo katika shughuli za uchumi. Kupitia *blueprint*, Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Pamoja na jitihada za Serikali, bado kuna mahitaji makubwa ya viwanda vya kuongeza thamani ya madini, kuongeza thamani ya mazao yetu vijijini na pia kuna changamoto za uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iendelee na msukumo wa kujenga viwanda vya mazao ili tuweza kuongeza thamani hapa nchini na pia kuzalisha ajira. Kutokana na neema ya kijiografia, nchi yetu inazalisha mazao ya aina mbalimbali ikiwemo zao la pareto na Tanzania inaongoza Afrika, pia ni wa pili duniani kwa uzalishaji wa pareto. Uwekezaji zaidi kwenye Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kuna fursa kubwa ya kuzalisha mbolea na hata viuatilifu kutokana na pareto inayolimwa hapa nchini. Serikali ichukue hatua za kutafuta wawekezaji wa viwanda vya

viuatilifu ambavyo mahitaji yake ni makubwa hapa nchini na hata soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nchi yetu ina neema ya madini ambayo ni malighafi ya kutengeza aina mbalimbali za mbolea. Madini aina ya *calcium* (chokaa ya kilimo) na *phosphate* inapatikana kwa wingi hapa nchini na malighafi muhimu kutengeneza mbolea aina ya *CAN* na *DAP* na hata *NPK*. Kuwepo kwa gesi asilimia ni fursa nyingine kwa viwanda vya mbolea aina ya *Urea* ambayo mahitaji yake ni makubwa sana Tanzania na duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na madini hayo kuna madini adimu duniani kama vile *NIOBIUM* ya *Pandahill* Mbeya ambayo kuna fursa ya kujenga kiwanda cha kuchakata hayo madini ili kutengeza *FERRONIIOBIUM* ambayo mahitajika yake ni makubwa hapa nchini na pia nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya *NIOBIUM* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR*, kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa.

Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *NIOBIUM* ambayo inapatikana milima ya *Pandahill*, Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahitaji kujiwekeka mikakati ya haraka (*quick wins*) ili kuhakikisha inakabiliana

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

na athari za kiuchumi kutokana *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium*, ajira 2,000 zitakozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs* 7,000. Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 (*US\$ 220 million*) ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 (*US\$ 22 million*) uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika (*Modern Manufacturing Plant and Smelter*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi (*skills transfer*) pia itakuwa itachangia huduma za kijamii (*Corporate Social Investment in Community*) na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana fursa za kijografia, napendekeza msukumo zaidi kwenye *EPZ* na *industrial parks* hasa kwenye bandari zetu na maeneo yanayozunguka viwanja vya ndege kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe kilichopo Wilaya ya Mbeya. Napendekeza Serikali ichukue hatua za haraka kubadilisha matumizi ya eneo ya iliokuwa *Tanganyika Packers* litumike kwa *EPZ* na *industrial parks* hasa kwa mahitaji ya viwanda mbalimbali ikiwemo vya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza mkakati wa Serikali kwa kuanzisha soko la bidhaa (*The Tanzania Mercantile Exchange - TMX*). Wizara ya Viwanda na Biashara iwe mstari wa mbele kuimarisha hili soko la bidhaa ambapo wauzaji na wanunuzi wanakutana na kubadilishana bidhaa na fedha katika mtindo wenye mpangilio na utaratibu maalum. Kuanzishwa kwa soko la bidhaa kutamwezesha mkulima kuweza kuuza mazao yake katika utaratibu unaoeleweka bila kulanguliwa. Pia soko la bidhaa linatupa mwanga na mwanzo mzuri wa kuboresha soko la madini kuwa sehemu ya *TMX*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri pamoja na timu yote ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa jitihada kubwa ya kufanikisha shughuli za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi, nina mchango mdogo; pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta nchini, bado hali ya upandaji wa bei ya bidhaa itafutiwe tiba. Manung' uniko ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niendeleo kukumbusha ujenzi wa kituo cha *SIDO* Ruvuma, Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa *Mwenyekiti*, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara (Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji) na Naibu wake (Mheshimiwa Exaud Kigahe) na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye sekta ya uwekezaji kwenye viwanda katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wa Kilimanjaro kihistoria ni mkoa ambao ulikuwa na viwanda vingi ambavyo vilichangia sana kuinua pato la wananchi wa mkoa huu na pato la Taifa kwa ujumla. Viwanda hivyo kwa sasa vingi vimefungwa kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kiwanda kilichokuwa kimepata mafanikio makubwa sana ni kile kiwanda cha kukoboa mpunga cha *Kilimanjaro Paddy Hulling Co. Ltd* kilichopo Chekereni – Moshi, katika Kata ya Mabogini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki kiko kwenye eneo ambalo linazalisha mpunga mara mbili hadi tatu kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

mwaka. Kiwanda hiki hakifanyi kazi tangu Septemba, 2014. Kiwanda cha kukoboa mpunga kilikodishwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahawa (*KNCU*) na baada ya kushindwa kukiendesha, mkoa ulimshauri Msajili wa Hazina kukirudisha Serikalini ili atafutwe mwekezaji mwingine anayeweza kukiendesha. Tayari Msajili wa Hazina amerejesha kiwanda hiki Serikali tangu tarehe 18/10/2018, lakini bado hajapatikana mwekezaji na shughuli zimelela. Kutokuwepo kwa kiwanda hiki kumeondoa fursa ya wakulima kupata bei nzuri ya mpunga na ajira kiwandani kwa wana Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha pili kilichopo jimboni kwangu na hakifanyi vizuri ni kiwanda cha bidhaa za ngozi Msuni kilichopo Kata ya Uru Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki kinamilikiwa na Kamati ya Maendeleo Kata ya Uru Kaskazini (*WDC*). Kina uwezo wa kuzalisha bidhaa mbalimbali za ngozi kama viatu, mikoba na mikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoomba mwaka jana, narudia tena kuiomba Serikali itume wataalamu wa *TIRDO* kwenye kiwanda hiki ili ushauri wa kitaalamu upatikane na kiwanda hiki kifufuliwe na kuunga juhudi za wana ushirika huu kwenye kukuza uchumi wao na wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Moshi Vijijini ni maarufu sana katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Kama Serikali itakuwa na mikakati ya kuhamasisha uwekezaji wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo, hii itasaidia kutengeneza ajira na kuongeza kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

Kwanza, Wizara itafute mwekezaji katika Kiwanda cha Kukoboa Mpunga cha *Kilimanjaro Paddy Hulling Co. Ltd* kilichopo Chekereni – Moshi, katika Kata ya Mabogini. Kiwanda hiki kinaweza kuwa ni chanzo cha

kusafirisha nje mchele ulioongezwa thamani na kuwapatia wakulima kipato na Taifa kwa ujumla.

Pili, Vyama vya Ushirika vilivyopo Jimbo la Moshi Vijijini vihimizwe na kuhamasishwa kuwa na viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo na kuyaongezea thamani ili kuzalisha bidhaa zinazotokana na kahawa, ndizi, mbogamboga, nafaka, mikunde, maziwa, asali, alizeti na mengine mengi.

Tatu, kama nilivyoomba mwaka jana, naomba tena Shirika la Utafiti wa Viwanda Tanzania (*TIRDO*) lishiriki kikamilifu kwenye kutoa ushauri wa kitaalamu kukufua kiwanda cha bidhaa za gozi Msuni kilichopo Kata ya Uru Kaskazini.

Nne, Serikali ianzishe programu maalumu itakayowashirikisha wadau muhimu wa viwanda kama vile *TIRDO*, *SIDO*, *TCCIA*, *VETA* na *CTI* ili watoe mafunzo ya kuhamasisha ujasiriamali wa viwanda Mkoani Kilimanjaro na hususani katika Jimbo la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote katika majanga mbalimbali na mafanikio katika nyanja za ustawi wa jamii, amani, uchumi, diplomasia na siasa za utashi mwema na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kuwapa pole nyingi wale waliopoteza wapendwa wao katika kipindi chote hadi leo hii, tunawaomba kwa Mwenyezi Mungu awapokee katika ufalme wake usio na mwisho mbinguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa namna ya pekee nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu ya awamu ya sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wa Jamhuri ya Muungano kwa jinsi inavyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe mchango wangu katika Wizara hii muhimu kwa ustawi wa uchumi wa Taifa letu. Serikali yetu ifanye mapitio ya blueprint ili kutathimini wawekezaji wa ndani na nchi ya nje kwa ajili ya kuona inatoa hamasa kwani changamoto kubwa inayosababisha nchi yetu kutokuhimili upandaji wa bidhaa na mfumuko wa bei ni uchache mkubwa wa viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi za ndani mfano wa wazi ni mafuta ya alizeti, sukari, kahawa na mengine, lakini husafirishwa nje ya nchi na baadaye kurudishwa ndani ya nchi baada ya kuchakatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ihamasishe uwepo wa wawekezaji wakubwa wa viwanda vya dawa, pembejeo za kilimo na uchimbaji wa mafuta na gesi kwani matukio ya janga la corona na vita vya Urusi na Ukraine na mengine mengi iwe ishara kwa Taifa letu kujifunza athari za majanga katika uchumi wa Taifa letu na kuepuka uagizaji mkubwa wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nadhani ni wakati muhimu sana Wizara yetu ione kupata tathimini ya viwanda vidogo 100 vilivyoanzishwa kwa kila Halmashauri kwani bado kwenye maeneo ya vijijini kuna malighafi nyingi za kutengeneza na kuchakata na kufungasha bidhaa za matumizi za majumbani kama subuni ili kupunguza mahitaji madogo madogo na kuchochea ajira mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

MWENYEKITI: Haya tunaanza sana na Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo dakika 10.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie nafasi hii kwa fursa hii uliyonipa; na mimi naomba nichangie. Kwanza nisema naunga mkono hoja. La pili, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri waliotupa kwa upande wa Serikali na nataka tu niwahakikishie kwamba kwa Wabunge kusema wazi mawazo yao inatusaidia sisi upande wa Serikali kuweza kutambua na kuelewa kwamba kwenye *planning* zetu tunatakiwa kuchukua hatua zipi za muda mfupi na za muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba hatujitoshelezi kwenye mafuta ya kula. Lakini ni ukweli kwamba upandaji wa bei ya mafuta ya kula unasababishwa na mambo makubwa mawili. Yapo yaliyopo ndani ya uwezo wetu na yapo ambayo yapo nje ya uwezo wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama nchi tunatumia wastani wa tani 650,000 kwa mwaka ya mafuta ya kula. Uwezo wetu wa uzalishaji ni wastani usiozidi tani 250,000 – 300,000; asilimia 70 ya haya mafuta tunayozalisha yanatokana na mafuta ya alizeti. Linapotokea tatizo duniani kama lilitokea la *COVID*, Ukraine, upande mmoja ni balaa lakini upande mwingine ni fundisho ambalo sisi kama taifa na watanzania; linatufundisha kwa sababu hapa tulipo ni maamuzi tuliyoyafanya kama taifa miaka ya 90; tulipoamua kuacha ku-*protect* sekta yetu binafsi na ku-*protect* viwanda vyetu *it was a policy* na ilifanywa na watanzania wote; na sheria zingine zilipita ndani ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo baada ya matatizo ya *COVID* nchi inajadili kwa nini hatuna mafuta ya kula? Baada ya matatizo ya Ukraine nchi inajadili kwa nini hatuna mbolea? Si kwamba hakuna rasilimali, Tanzania ilikuwa na Tanzania *Fertilizer Company* tuliama; kwa hiyo kama tumeamua kama nchi kutubu kurudi kwenye misingi *let us take a responsibility as a country*; isiwe kuinyooshea kidole Serikali, isiwe kuinyooshea kidole Serikali, Serikali ilitekeleza maamuzi yaliyopitishwa na Bunge hili hili na sheria zilipitishwa humu humu ndani. Tuliama kwenda kwenye mfumo wa uholela; tukaua mambo yetu ya msingi kama nchi. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inachukua hatua gani? Moja, tunachukua *two policy direction* ambazo tunafanya Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha. Cha kwanza, mwaka huu tumefanya *pilot* ya kugawa mbegu kwa mikoa mitatu; tumegawa kwa ruzuku. Nataka niseme na sisi tuwe wakweli kwa sababu siku ya mwisho *we will all die*, tutakwenda kuhukumiwa kwa Mungu. Dhana ya kufikiri Serikali haina jukumu la kulinda sekta binafsi kwa ku-*protect* viwanda vyake vya msingi ni dhana potofu. Kwa sababu sasa hivi *all over the country* wanainyooshea kidole Serikali *and we forgot* kuwa ni sisi ndio tuliamua kutokulinda viwanda vyetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua ku-*protect* na Serikali ya Awamu ya Tano ilianza; tume-*protect* sekta ya sukari kwa uweo wa Mwenyezi Mungu 2025 tutajitosheleza. Serikali sasa hivi kuhusu viwanda vidogo vidogo vya sukari tunafanya nini? Wizara kupitia Bodi yetu ya Sukari kwa kushirikiana na TEMDO tunatengeneza *portal types small industries* za ku-*process metric tons* 10 kwa siku ya miwa ambayo itatupatia tani 24 kwa mwezi ili tuweze kuwapa vyama vya Msingi vya Wakulima. Anayegharamia ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kazi hii inafanywa na TEMDO na tutatengeneza hivi viwanda vidogo tutawagawia wakulima ili AMCOS katika ngazi za chini waweze ku-*process* sukari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya nini kwenye mafuta ya kula? Tumegawa mbegu tani 3,000 na mwaka huu kwa uwezi wa Mwenyezi Mungu mkipitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo tutagawa *certified seeds* tani 5,000 kama ruzuku kwa wakulima. Lakini kugawa mbegu peke yake hakutoshelezi lazima viwanda viwe *competitive*; tumejadiliana na Wizara ya Fedha tunachukua hatua za kikodi ili kuvilinda viwanda vyetu vya ndani ili viweze kuzalisha mafuta ya alizeti na siku ya mwisho yaende sokoni. Hatutomaliza tatizo la kujitosheleza mafuta kwa mwaka mmoja; lakini kwa uwezo wa Mungu ndani ya miaka mitatu tutajitosheleza na tutakuwa na mafuta ya kutosha ya alizeti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana sana suala la mafuta ya kula; hatua ya pili tunachukua kwenye *palm oil*. Ukienda kwa mama ntilie hakaangi vitumbua kwa kutumia mafuta ya alizeti, anatumia mafuta ya mchikichi; ukienda kwa mama ntilie anatumia mafuta ya mchikichi. Sisi kama Serikali hatua tunayochukua wakati tuna-*develop* kwa muda mfupi mafuta ya alizeti *long term* tunakwenda kwenye *palm*. Tumeanza kuwapa wawekezaji wakubwa maeneo makubwa kwa ajili ya kulima mchikichi. Kwa muda mrefu mchikichi na lazima tuelewe kuna kitu kinachoitwa *economies of scale*. Mchikichi hauwezi kuwa *profitable* kwa kulima heka moja halafu tukadhani kwamba yule Muha wa Kigoma anaye-*crush* mchikichi na kuzungusha kwenye pipa siku ya mwisho yale mafuta yataweza kuwa *competitive* sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukua hatua gani? Tumepata wawekezaji wakubwa ambao tunawapa 10,000 *hectares*; moja tunampa Bakheresa hekta 10,000 *down stream* ya Rufiji kwa ajili ya kuweka michikichi, tuta-*develop* pembeni yake *small scale farmers* yeye ndiye atakayenunua na ku-*crush* ndipo pote duniani wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kule Kigoma tumegawa michikichi, Serikali inachukua hatua gani? Tutaweka viwanda vidogo katika eneo la Kigoma Manispaa ili miche tuliyogawa mwaka jana na mwaka juzi ambayo inakaribia ku-*mature* iweze kuweza kupata sehemu ya *crushing*. Nini nataka nimalizie, mimi nataka niseme jambo moja; suala la kilimo na kujitosheleza kwenye masuala ya msingi hasa mafuta ya kula, *fertilizer*, sukari ni suala la lazima. Tunawaomba Waheshimiwa Wabuge waiunge mkono Serikali kwenye hatua tunazoanza kuchukua kuanzia mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili suala la mbolea; ili viwanda viweze kupata rasilimali lazima mkulima azalishe; gharama za uzalishaji zikiwa kubwa mkulima hawezi kuzalisha na hata atakachozalisha kiwanda hakitaweza kununua. Kwa hiyo, ni lazima tukubali kama nchi tuanze kutoa ruzuku kwenye

maeneo ya msingi na tuwaombe Waheshimiwa Wabunge Serikali inachukua hatua ya kupunguza gharama za riba, Serikali itachukua hatua za kikodi kuanzia mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya kulinda *industries* ambazo ni muhimu; Serikali itachukua hatua ya kutoa ruzuku kwenye mbegu za mazao ya mafuta. Tutatoa ruzuku kwenye mbolea ije jua ije mvua tunawaomba mtuunge mkono kwenye hatua hizi; tuache kushauriwa kwamba Serikali haitakiwi ku-*intervene* kwenye maeneo ya msingi ni lazima tu-*intervene this is the small economy*, sekta yetu binafsi bado ni changa inahitaji *Government intervention*. Tutakapochukua *Government intervention* tunawaombeni mtuunge mkono kwenye masuala ya msingi ya kutoa *subsidy*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo; sasa namkaribisha Naibu Waziri, Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Naibu Waziri karibu.

NAIBU WAZIRI, UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai kuweza kusimama hapa mbele na kuwasilisha bejeti hii; lakini kwa namna ya pekee nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuendelea kufanya kazi kama Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nipende kushukuru sana michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia kwa mtazamo chanya kwenye bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuendeleza kutimiza adhama ya ujenzi wa uchumi wa Viwanda nami nasimama hapa ili niweze kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi kubwa

na umakini ambao anaoufanya katika kuendelea Sekta hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimwia Mwenyekiti, bajeti iliyowasilishwa imebeba dhamira kuu ya kuendeleza kasi ya uwekezaji na ujenzi shirikishi na unganishi wa Uchumi wa Viwanda kwa kutambua nafasi ya Sekta Binafsi; kama ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza kama injini ya ujenzi wa Uchumi wa Viwanda na shughuli za ubia kwa Sekta Binafsi ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa mfumo huu wa maboresho na mengine yanayoendelea nchini likiwemo kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya biashara kwa maana *Blue Print* unalenga kuboresha mazingira ya biashara na kushushia ari ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na kuleta maendeleo endelevu katika nchi na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya awali na mimi niweze kuchangia kidogo kwanza kwenye hoja zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira katika kuchangia bajeti hii. Kulikuwa na hoja kuhusu Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara ya *TanTrade* ambayo imechangiwa pia na Wabunge wengi sana, kuhusu kuona namna gani tunaweza kuisaidia ili kuhakikisha inatimiza wajibu wake kwa kufanya kazi ya kutafuta masoko ya bidhaa hasa mazao ya kilimo na bidhaa nyingine. Serikali inafanyakazi kubwa kuhakikisha tunawezesha taasisi zote ikiwemo hii ya *TanTrade*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika bajeti hii tunayoendelea nayo sasa tulikuwa tumewapa fedha kidogo lakini mwaka huu tumeongezea kufikia bilioni 1.8 hii maana yake ni kuiwepo kwa dhamira njema ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha masoko ya bidhaa na hasa mazao ya kilimo yanapata masoko ya uhakika kwa kuhakikisha *TanTrade* inafanyakazi yake vizuri. Lakini Serikali itaendelea kuweka fedha zaidi kuhakikisha *TanTrade* inafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kulikuwa na hoja kuhusu uandaaji wa kanzidata ya viwanda. Ni kweli Kanzidata ya viwanda ni moja ya matokeo ya utafiti na utambuzi wa viwanda ambayo huwa ni fursa kwa uwekezaji na wa rasilimali inayopata hapa nchini.

Kwa hiyo, kanzidata ni kweli itakuwa na taarifa sahihi za viwanda ikiwemo maeneo viwanda vilipo, ukubwa na uwezo wa viwanda hivyo na ajira ambazo zinatokana na viwanda hivyo. Lakini zaidi itaweza kutusaidia kujua malighafi zinazotakiwa kwa ajili ya kuzalisha bidhaa katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa taarifa hizo zitatusaidia pia kuona namna gani tunajua wapi kwa kuwekeza kwenye maeneo yapi, pia ambapo tunaamini yataleta tija. Sasa Wizara kupitia *TIRDO* tumeshaanza kazi hiyo kwa kushirikiana na taasisi zingine kama vile Ofisi ya Rais, *TAMISEMI*, *NBS*, *BRELA* na *SIDO* wanaendelea na uhakiki wa kukusanya takwimu za taarifa mbalimbali ambazo zitajumuishwa kwenye kanzidata ya viwanda katika Mikoa mbalimbali hapa nchini na sasa wameanza katika Mikoa ya Kanda ya Mashariki ikiwemo Morogoro na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia kwenye Kamati kuhusu uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji hapa nchini, ambao pia imechangiwa pia na Waheshimiwa Wabunge wengi. Wizara kupitia Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) inakamilisha mfumo wa kielektroniki wa kutoa huduma ya mahali pamoja kwa wawekezaji (*Tanzania Investment Electronic Single Window*), ambayo itasaidia kuhakikisha tunaondoa baadhi ya changamoto na kupunguza urasimu usio wa lazima ambao umesababisha ucheleweshwaji kwa upatikanaji wa vibali kwa wawekezaji ikiwemo kujaza fomu nyingi na kujirudiarudia kwa sababu ya taasisi nyingi ambazo zinafanya kazi zinazofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni hoja chache kutoka kwenye Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie kidogo kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika bajeti hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambayo aliongelea kuhusu umuhimu wa kuwezesha Bodi ya Maghala ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa uhakika na kwa ufanisi zaidi. Ni kweli nasi Wizara na Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha tunawezesha Bodi hii iweze kufanya kazi yake. Kwa sasa hivi inasimamia baadhi ya shughuli lakini pia tutaleta nadhani maboresho ya Sheria kuona sasa inasimamia maghala yote nchini ili yaweze kufanya kazi zake vizuri, lakini tumeendelea kuwawezesha kwa kuwapa fedha zaidi kila mwaka ili waweze kukamilisha majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alisema hoja ya Bodi hii ihakikishe inaweza kujenga maghala kwenye vijiji na maeneo mengi. Nia ya Serikali ni kuona sasa tutashirikisha sekta binafsi ili nao waweze kufanya kazi zao vizuri lakini pia na sisi kama Serikali tutaendelea kuwezesha ujenzi wa maghala hayo maeneo tofauti tofauti na hasa vijijini ambako ndiko kuna haja kubwa ya kuwa na maghala haya ili wananchi waweze kuhifadhi mazao yao yawe katika ubora unaotakiwa lakini pia kuweza kudhibiti kupata bei bora ya mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Subira Mgalu kuhusu *SIDO* kuwezesha mitaji ya fedha lakini pia kuwezesha na vitendea kazi. Ni kweli *SIDO* ambayo ndio inahudumia viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuona sasa tunaimarisha sekta hii ya viwanda vidogo vidogo ili viweze kusaidia wananchi wengi zaidi kwenye ngazi ya chini ambako ndiko wananchi wengi wanashiriki katika kukuza uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, tutaendelea kuwawezesha *SIDO* na kuhakikisha teknolojia muhimu katika maeneo tofauti

mikoani mpaka kwenye Halmashauri ili angalau zisaidie maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya kuhakikisha kufanya tathmini ya vile viwanda mia moja vya kila Halmashauri ambavyo tulikuwa tunaendelea navyo. Ni kweli tutaendelea kufanya zoezi hilo la utambuzi wa viwanda vile na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vingine ili kuhakikisha kila Mkoa unapata fursa ya kuongeza thamani hasa kwenye eneo hili la mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine pia ya kuona namna gani tunaendeleza kuhakikisha tunahamasisha ujasiriamali. Kama nilivyosema *SIDO* ndiyo wanasaidia sana katika eneo hili lakini pia na vyo vingine kama *VETA* na Taasisi zingine *TCCIA* na *CTI* ambao wapo kwenye sekta binafsi kuhakikisha tunawawezesha wajasiriamali katika elimu kwa maana ya ujuzi lakini pia teknolojia lakini na mitaji kuhakikisha nao wanashiriki vizuri katika kuendeleza sekta ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kusema tena naunga mkono hoja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, tuunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri ili kuhakikisha Wizara inaweza kutimiza majukumu yake katika Mwaka, 2022/2023. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Exaud Kigahe Naibu Waziri, Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mchango huo. Sasa nimkaribishe mtoa hoja ambaye ni Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaju. *(Makofi)*

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 6 Mei, 2022 niliwasilisha katika Bunge lako Tukufu hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ikiainisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka, 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru, Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ambavyo mmeongoza na kusimamia vyema majadiliano ya bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao waliyotoa kwa njia ya kuzungumza na maadhishi pia, maoni na ushauri wenu tumeuchukua kwa ajili ya kuufanyia kazi ili tuweze kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kuwa ninatambua na kuthamini dhamira na nia njema iliyotawala mjadala huu ambao kimsingi ulilenga kuboresha mikakati na mbinu za kisekta, zitakazotekelezwa katika mwaka 2022/2023 na hata kuelekea mbele zaidi na hivyo kutoa mchango unaotakiwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini na Makamu Mwenyekiti wetu Eric James Shigongo Mbunge wa Buchosa, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na ushauri mzuri waliotupatia kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi ndani ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau Mjumbe wa Kamati, kwa kuwasilisha vema Taarifa ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti, hongera sana. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kuanzia mwanzo mpaka mwisho na kipekee kabisa, naomba pia nimshukuru Kaka yangu Mheshimiwa Mohamed Hussein Bashe Waziri wa Kilimo kwa kuchangia hoja hii na kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninawashukuru Watendaji wote ndani ya Wizara yetu wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kuweza kufanya kazi usiku na mchana, hadi leo tunaelekea kuhitimisha mjadala huu wa hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea pongezi nyingi za utendaji wa Wizara na Taasisi zake kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge nasi tunaahidi kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa ari zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tumepokea michango mingi ambayo ni chachu katika kuleta maendeleo ya uchumi wa nchi yetu, hususani kupitia sekta yetu ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Napenda kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge kuwa maoni na ushauri wenu na maelekezo ya Bunge hili katika kujadili bajeti ya sekta hii tutayazingatia kuyafanyia kazi ikiwemo kutoa mrejesho wa utekelezaji. Aidha, kutokana na muda mfupi tulionao hadi kuhitimisha hotuba hii, maelezo na majibu ya kina ya michango mbalimbali yameandaliwa na tutayawasilisha kwa maandishi kwa Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya bajeti ya Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni Wabunge 29 na kati ya hawa Waheshimiwa Wabunge 23 wamechangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge Sita wamechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja

zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili hoja hii niliyowasilisha kama ifuatavyo: - (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako niruhusu nijikite katika hoja moja au mbili ambazo ni msingi mkubwa wa mjadala huu wa siku hizi mbili za kujadili hotuba ya bajeti yetu. Hoja yenyewe inaweza kuwa imebeba michango yote ya Waheshimiwa Wabunge nayo ni hoja iliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kuhusu hali ya sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, lakini ikiunganishwa na hali inayoendelea duniani hali ya mfumuko wa bei katika bidhaa mbalimbali na mwishoni ikionekana kama Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inaendeshwa bila maono wala dira naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi duniani iliyofikia hatua ya juu ya maendeleo bila kuwa na mageuzi ya uchumi wa viwanda. Hata hivyo, nadharia ya maendeleo ya kiuchumi (*Theory of Economic Development*) inabainisha kwamba ipo misingi muhimu misingi mikuu ambayo nchi ama Taifa hutakiwa kuwanayo ili kufikia hatua yoyote ile ya maendeleo. Misingi hiyo ni uwepo wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya shughuli endelevu za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea kwenye nadharia ya uchumi wa miundombinu (*The Economics of Infrastructure*) inatueleza miundombinu hii wezeshi uwekezaji wake ni mkubwa na hakuna Taasisi ama Sekta binafsi yoyote yoyote ambayo ipo tayari kuwekeza kwenye miundombinu, lazima miundombinu hii wezeshi iwekezwe na Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu hii wezeshi ni pamoja na miundombinu ya barabara ni pamoja na miundombinu ya usafirishaji wa reli, usafirishaji wa anga, miundombinu ya afya, miundombinu ya elimu yote hii lazima iwepo kama tunataka kuona matokeo makubwa ya uchumi wa viwanda ndani ya Taifa lolote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi yetu Tanzania ilikuwa ni muhimu sana tulipopata uhuru mwaka 1961 kuwa

na mipango ya muda mrefu na mipango ya muda mfupi. Nichukue fursa hii, kuwapongeza sana Viongozi wetu wa Serikali ambao wote wametokea Chama cha Mapinduzi kuanzia Serikali ya Awamu ya Kwanza Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere nampongeza kwa dhati ya nafsi yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee wetu Alhaji Ali Hassan Mwinyi nampongeza kwa dhati ya nafsi yangu alifanya makubwa kuhakikisha, nadharia hizi za uchumi zinafikiwa na Taifa letu linanufaika na mapinduzi ya viwanda. Nampongeza sana Mzee wetu Hayati Mkapu alifanya makubwa. Nampongeza sana Rais wetu mstaafu wa Awamu ya Nne Jakaya Mrisho Kikwete alifanya makubwa kuhakikisha Taifa letu linanufaika na uchumi wa viwanda.

Nampongeza sana Hayati Dkt. John Pombe Magufuli amefanya makubwa na sasa nampongeza sana Mama mlezi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan anafanyakazi kubwa kuhakikisha yale yote yaliyofanywa na watangulizi wake yanazaa matunda yanayotakiwa. Pongezi nyingi na niliombe Bunge lako Tukufu tusimkatishe tamaa Rais wetu anafanyakazi kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ipi ilikuwa dira yetu baada tu ya kupata uhuru. Baada ya kupata uhuru dira yetu ilikuwa ni kuwa na Taifa huru katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hivyo, ili tuweze kufika huko kama Taifa ilitulazimu tuanze hatua moja kwenda hatua nyingine na ndipo aliposema Mheshimiwa Waziri wa Kilimo viwanda vilijengwa katika Serikali ya Kwanza ni sahihi kabisa, lakini kuna kiwanda kilicho jengwa eneo moja la nchi unazalisha bidhaa ambazo hakuna miundombinu ya kupeleka sokoni unakwenda kuzalisha tunachokiita *botanic inflation*. Kwa hiyo, kifo kile kilikuwa ni kifo cha kiuchumi na wala hatutakiwi kujilaumu na kwa sababu tuna Serikali makini, ndio maana tukarudi kwenye nadharia zote za kiuchumi na sasa tuko sehemu sahihi ya kunufaika na mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo dunia nzima ipo. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalisemwa sisi watanzania kweli tulalamike kuhusu mafuta kutoka Ukraine, mafuta kutoka Malaysia ambayo yameshindwa kufika nchini ni sahihi. Kwa sababu, tulianza na utekelezaji wa mipango mingine huko nyuma, naomba nianzie na Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano tulioanza kuutekeleza mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2015/2016. Mpango huu ullenga kufungulia fursa fiche za ukuaji wa uchumi baada ya kuwa tumesoma tumerudi kwenye *Structural Adjustment* tumeona haifanyikazi, wachumi wa Taifa hili wakafanya kazi yao na sasa tukaanza mwelekeo sawasawa wa kwenda kunufaika na mapinduzi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ulitaka kuhakikisha kuwa Taifa letu linakuwa na miundombinu sahihi kwa ajili ya kuwezesha shughuli zingine za maendeleo kuelekea kwenye uchumi wa kati na wa juu. Ni katika kipindi hiki ndipo tulipoona kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona ukarabati wa reli ya kati yenye urefu wa kilomita 2,707 ambapo huko nyuma tuliona matatizo makubwa ya miundombinu hii lakini tulikarabati na mwendo ukaendelea. Tukahakikisha kuna jengo la kukarabati kilomita 2,775 za barabara za lami kwa mara ya kwanza ndani ya Taifa letu tukielekea kuufungua uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaona maboresho makubwa katika Bandari ya Dar es Salaam ambako uwezo wa kuhudumia shehena ya mizigo uliongezeka kwa kiwango kikubwa. Tukaona kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kutoka megawati 900 mwaka 2010 hadi megawati 1,246 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukazalisha chakula cha kutosha hadi asilimia 125 ya chakula kikazalishwa. Tukaona miundombinu ya elimu shule za kata zikajengwa kwenye kila Kata ndani ya Taifa letu. Tukaimarisha miundombinu ya afya na lishe katika ngazi zote kwa wakazi wote wa Mijini na Vijijini.

Huwezi kuwa na Tanzania ya viwanda kama huna jamii ambayo iko imara kiafya na ambayo imeelimika. Hii ilikuwa ni mpango wa kwanza wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Pili wa Maendeleo ambao ulisemwa hapa Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa ya viwanda; viko wapi viwanda? Viwanda tunavyo na nimetaja kwenye hotuba ya bajeti yangu. Mpango wa Pili wa Maendeleo ulikuwa na dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Lengo kuu la pili lilikuwa ni kurekebisha mapungufu yote ya mpango wa kwanza ili tuweze kuendelea kutembea mguu sawa kuelekea mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwenye mpango huu ndipo tulipoona Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na msaidizi wake Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, tukianza ujenzi wa reli ya kisasa ili kuhakikisha sasa viwanda vyote vilivyojengwa vikizalisha bidhaa ichukue muda mfupi bidhaa hizo kufika bandarini na kusafirishwa nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mradi mkubwa wa kuzalisha umeme. Huwezi kuwa na viwanda kama huna umeme wa kujitosheleza. Tunao mradi mkubwa wa umeme unaokwenda kuzalisha megawati 2,115 ambao hatuna muda mrefu mradi huu unakamilika. Ni maandalizi ya uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, moja ya hati za makubaliano tulizosaini ni mkataba wa kibiashara kati ya Jiji ya Dallas na nchi yetu ya Tanzania. Jiji la Dallas liwe kama lango la biashara ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania kwenda kuuzwa katika Bara la Amerika yote Kaskazini na Kusini, lakini Tanzania kiwe kama kituo kikuu cha biashara kwa Afrika ya Mashariki, kwa Afrika ya Kusini na Nchi za Afrika ya Kati. Biashara zote zinazotoka duniani zipite Bandari ya Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo tunayoyafanya kuelekea uchumi wa viwanda na kupitia utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo tukaona mradi wa kufufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) inafanya kazi ndani ya nchi na nje ya nchi. Huwezi kuingia mikataba ya biashara na wenzako, wenzako wakaleta ndege zao wewe usifanye hivyo, hapana. Moja ya kipengele kwenye mkataba huu ni kuwa na mkataba mwingine mdogo (*Open Skies Agreement*), niishukuru Wizara ya Uchukuzi inahitimisha mkataba huo ili sasa na sisi ndege zetu ziweze kuruka kuelekea duniani kupitia Dallas. Haya yote yamewezekana kwa sababu tumetekeleza mpango wa pili wa maendeleo tukifungua zile fursa fiche, miundombinu wezeshi kwa ajili ya uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya msingi, Mpango huu wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pia ulijikita katika kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini, hususan katika sekta za kilimo, madini na gesi asilia na uzuri takwimu huwa zinaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya viwanda utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo tulifikia asilimia 105 ya malengo tuliyokuwa tumejiwekea. Kwa mara ya kwanza tukaona mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la Taifa ukifikia asilimia 25.1, ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kasi ya ukuaji wa shughuli za uzalishaji iliongezeka kutoka asilimia 5.2 hadi asilimia 8.5, huku tukiona mchango wa sekta ya madini ukikua kwenda kufikia asilimia 12.6 kutoka asilimia 6.9. Hii ni kwa sababu miundombinu wezeshi yote ilishafanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunatekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano tulioanza kuutekeleza mwaka 2021/2022 na tunakwenda kuhitimisha mwaka 2025/2026, ambao ni muendelezo wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na lengo lake kuu sasa ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu wetu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mmesema vizuri sana, lazima viwanda hivi vitambue watu wetu nini walichonacho. Ndio maana sasa baada ya kuona miundombinu wezeshi yote imekamilika nchi yetu imefunguka kwa miundombinu. Bidhaa itakayozalishwa kwenye kona yoyote ya Taifa letu ina uwezo wa kusafiri kwenda eneo lingine lolote ndani ya Taifa letu kwa muda mfupi. Ndani ya mpango huu ndio tunamwona kiongozi wetu makini, jasiri, Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, anaelekeza bajeti kwenda kwenye sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Bashe, amesema vyema. Hotuba ya bajeti yake inakwenda kuongezeka kwa kiwango kikubwa. Hiyo yote ni kuwezesha viwanda vyetu vipate malighafi tayari kwa uzalishaji ili tuweze kusafiri salama kwenye safari ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imefunguka kama nilivyosema kwa miundombinu yote ya msingi kuelekea uchumi shindani na wa viwanda. Pongezi nyingi kwa Serikali yetu ya Awamu ya Sita na Serikali nyingine zote ambazo zimeongozwa na wazalendo wa Taifa letu waliojua vipaumbele vya Taifa letu kuelekea kwenye nchi ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ndio maana tunaona sasa jitihada kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais wetu ni kueleza ulimwengu Taifa letu liko tayari sasa kwa safari ya kimaendeleo. Tuko tayari na wawekezaji tumefungua milango ili waje kuwekeza kwenye maeneo yote ya kiuchumi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mikataba ambayo tumesaini, hati zote za makubaliano 44 zote zinawaelekeza wawekezaji kuja kuwekeza katika sekta za uzalishaji, katika sekta za viwanda. Ndio maana mpaka kufika mwaka 2025 tutakuwa hatuna tena upungufu wa sukari nchini Tanzania, tutazalisha kutoka Tanzania, kutoka kwenye viwanda vidogovidogo na viwanda vikubwa na jitihada hiyo ni pamoja na uwekezaji kwenye eneo la Mkulazi ambalo Waheshimiwa

Wabunge wamesema na tayari mwekezaji yuko *site* anafanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakwenda kutumia teknolojia zote, teknolojia za kati, teknolojia za juu, ili kuhakikisha viwanda vidogovidogo, vya kati na vikubwa vinawekezwa. Ndio maana tuna kongani za viwanda kule Kitaraka, Manyoni, lakini tuna kongani za viwanda pale Kwala, Kibaha na tuna kongani za viwanda hapa Nala, Dodoma. Tunachotaka kufanya ni kuihudumia dunia kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wametusema kwamba, tuongezewe fedha, lakini wamekiri sisi ni Wizara inayoratibu uwekezaji na viwanda. Uwekezaji na viwanda hivi upo kwenye sekta nyingine za kiuchumi na tunafanya kazi kwa karibu zaidi na sekta zote; sekta ya madini, sekta ya kilimo, sekta ya fedha tunafanya kazi kwa karibu kuhakikisha haya yote yanafanikiwa. Tuko kwenye majadiliano na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuona viwanda vilivyopo kwenye mifugo na uvuvi tunavipaje kipaumbele ili vinufaike na mafanikio makubwa haya. Kwa hiyo, niwatoe hofu tunafanya kazi hii kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niseme tu Taifa letu lina dira ya muda mrefu na lina dira ya muda mfupi. Mipango yote hiyo inapitishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji. Kikubwa niwaombe Waheshimiwa watuunge mkono ili tuweze kuyatimiza haya yote mazuri tunayoyapanga kwenye sekta hii ya uwekezaji, viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nianze na jambo hili na moja dogo la pili ambalo napenda kulisemea kabla muda wangu haujaisha ni mradi wa kimkakati wa Liganga na Mchuchuma. Tumesikia Bunge lako limesema na limekiri ni mradi wa muda mrefu. Tunafanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuona tunapohitimisha

mjadala na mwekezaji wetu Taifa letu linaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze timu yetu ya kitaifa ya majadiliano imefanya kazi yake nzuri na sasa jambo hili liko mikononi mwa Waziri wa Uwekezaji na Mwanasheria Mkuu wa Serikalim. Tunaliahidi Bunge lako Tukufu tunakwenda kulihitimisha. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ludewa, ndugu yangu Mheshimiwa Kamonga, alitahadharisha kuhusu mgongano wa sheria mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inafanya kazi kuona hakuna mgongano wa sheria hizi mbili, Sheria ya Ardhi pamoja na Sheria ya Uthamini ili tuweze kufika hatua njema kwa ajili ya wananchi wetu na wananchi wetu waweze kufanikiwa. Jambo ambalo naweza kuahidi ni kwamba, Wizara yangu pamoja na Mthamini Mkuu wa Serikali tutafanya ziara na kuongea na wananchi wa vijiji hivyo viwili ili tuweze kuhitimisha jambo hili kwa mafanikio makubwa kati ya Serikali, wananchi wetu, pamoja na mwekezaji wetu. Hivyo, nimtoe shaka Mbunge, tuko tayari na muda mfupi mradi huu utaanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda tena kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii. Niwaombe tu tuendelee kushirikiana katika kuwatumikia Watanzania katika kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zinazofanywa na Serikali yetu kupitia Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, zinatuhusu sisi sote. Tumemsikia jana Mheshimiwa Rais akisema ametusemea vizuri Watanzania; sisi ni wakarimu, wawekezaji wamemsikia wanakuja kwa wingi. Naomba tuwapokee na tushirikiane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja, wa kutengeneza mabilionea kutoka ndani ya Watanzania waongezeke zaidi

na wanaanza na sisi Waheshimiwa wawakilishi wa wananchi. Sisi Wabunge tushiriki, Taifa letu limefunguka na tunasema Tanzania *is ready to take off*, lazima na sisi tuwe ndani ya safari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie pia kuwa, Wizara yangu itaendelea kulea na kuisimamia sekta binafsi ya Tanzania. Hakuna Taifa lililofanikiwa bila sekta binafsi. Ndio maana viwanda vingi kwa asilimia 90 vinashikiliwa na sekta binafsi.

Mimi nasafiri na sekta binafsi kama Waziri mwenye dhamana. Mheshimiwa Rais wetu kwenye safari zake zote anasafiri na sekta binafsi ili sekta yetu binafsi ishindane ndani na nje ya Taifa letu. Hivyo, tusafiri kwa pamoja kwenye safari hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na hoja imeungwa mkono.

Katibu tuendeleo.

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, ndc – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

MWENYEKITI: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, ndc – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida. Ukurasa wa 287.

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 44 - Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management.....Sh. 15,585,607,763*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge katika Kifungu hiki cha Mshahara nimepata jina moja, Mheshimiwa Condester Sichalwe.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kama nilivyotoa maelezo yangu wakati nachangia hoja, nilimpa Taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba nakusudia kushika shilingi yake kama hatanipa ufafanuzi kwenye hoja yangu ambayo nilikuwa nimechangia.

Nilikuwa nimetoa ushauri kwa Serikali, kutokana na pombe hizi za kienyeji zinawasaidia Watanzania wengi, *especially* akinamama na bibi zetu na walezi wa familia hizi, iundwe bodi kama ambavyo Wizara ya Kilimo imeunda Bodi ya CPB kwa ajili ya kusimamia mazao yote na nafaka mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi hii na yenyewe kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara iweze kuzitambua pombe zote za kienyeji ambazo ziko hapa nchini, lakini wawasaidie kufanya utafiti, lakini pia kuwasaidia kupata ithibati na kusaidia ku-*regulate* ubora wa pombe ambazo wanazona hazifai kwa matumizi ya binadamu. Watupe hata ufafanuzi kwa nini gongo inafaa na haifai na kwa nini Jack Daniel na hizo Godonson zinafaa? Je, wamepima wakaona wanaweza wakapunguza kiwango kipi cha *alcohol*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara watuambie ni namna gani watawasaidia akinamama hawa kuwawezesha kwa sababu, mkopo wa asilimia 10 ambao asilimia nne wanapata akinamama hauwatoshi, lakini pia mambo ya kuwazuia watumiaji wa pombe hizi kwa mtutu wa bunduki, tuwachie viongozi wetu wa kidini wao ndio wana lugha nzuri ya namna gani wanaweza wakawaambia wananchi wakaamua kuacha kutumia pombe au maelezo kutoka kwa Daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi. Yeye kama Waziri wa Viwanda na Biashara atasaidiaje pombe hizi za kienyeji ambazo zimewatoa akina Profesa Kitila Mkumbo wengi na Wabunge wengine ambao wako hapa ndani na wafanyabiashara matajiri na hizo baa ambazo zinafanya vizuri na Serikali inachukua kodi.

Naomba ufafanuzi, usiponipa maelezo ya kutosha nimekusudia kushika shilingi au atoe *commitment* wananchi wa Kijijini kule Momba na maeneo mengine hapa Tanzania ambao wanaishi kwa kutumia pombe za kienyeji, waone Serikali imekusudia kuchukua hatua kuwasaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Simbachawene.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, nimesimama kutoa ufafanuzi wa suala hili kwa sababu, ni suala mtambuka. Linaunganisha Wizara nyingi zinazoguswa na suala la pombe za kienyeji na hususan gongo anayoisema, ambayo sababu za kuizuia kwa mujibu wa sheria zimetokana na historia yake. Hata hivyo, tunaruhusu pombe nyingine zote ambazo hazina madhara ya haraka kwa binadamu, lakini tunazikataza hizi kwa sababu ya namna ambavyo viwango vyake vya kilevi si rahisi kuvipima kwa namna inavyotengenezwa kiholela inakuwa ni ngumu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tofauti sana kuruhusu pombe ya kilevi kikali kuitengeneza kwenye kiwanda ambako utaalim husika unaweza ukatizamwa na pale unapokwenda kuruhusu kila mtu akaitengeneza kwa sababu, kila kabila ina gongo yake, kila jamii ina gongo yake, kuna pombe kali yao wanayokunywa. Sasa tukisema tunaruhusu, basi ni lazima tuandae maandalizi ya msingi makubwa tu ya kuhakikisha kwamba, tunaweka namna ya udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hata hapa hapa nchini viko viwanda vinavyotengeneza. Kwa mfano, *K-vant*; ile ni *gin*, ni kama Konyagi, zote zinatengenezwa hapa Tanzania. Zinazotengenezwa na baadhi ya jamii kwa mfano wanaotumia mimea na zile zinazozalishwa ni sawa na Konyagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa kiwango cha ule ulevi kama binadamu atatumia ndicho kinachotusumbua. Ndiyo maana tunaona madhara yake ni makubwa kwa watu wetu na hasa wa kipato cha chini endapo wataruhusiwa. Ndiyo maana tuliporuhusu viroba vilitupa shida, tulipoteza nguvu kazi ya Taifa kubwa sana na vijana wote mtaani walikuwa kila mmoja ni *fashion* ya kutembea na viroba kwa sababu ya ile *package*. Tukaongeza ukubwa wa *package* ili iwe siyo rahisi kuweza kuvitia mfukoni na kunyonya. Jamii ilishaharibika sana, hasa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu, hoja ya Mheshimiwa Mbunge inaeleweka na tumekuwa tukipata hoja kama hizi zikijirudia rudia ndani ya Bunge. Wacha tuichukue kama Serikali, halafu tufanye tafakari, tufanye tathmini. Tumeona ametumia nguvu kubwa kweli kweli, nami naamini nguvu hii aliyoitumia ni kwa sababu ya uhalisia tunaouona sisi sote kwenye jamii, kwamba wapo watu ambao kila siku unawakatama, wanarudia kufanya; unawakamata wanarudia kufanya; ni *habitual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tufike hatua kama Serikali tuwe na majibu na maelezo yanayofaa ili jamii kama ni kuacha tuache, kama ni ku-*modernize*, basi

tu-*modernize*. Kwa hiyo, hili haliwezi kuwa la Wizara ya Viwanda na Biashara peke yake, bali na Serikali nzima kwa maana linagusa afya za watu na mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu, nakushukuru sana kwa mawazo yako, acha tuyachukue tuone tunavyoweza kujadiliana na tutawashirikisha Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Condester Sichalwe.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kutokana na upana wa hoja hii, namna kule ninakotoka ambavyo nimeona wananchi imewasaidia, nataka kutoa hoja Wabunge wenzangu wanisaidie tuijadili ili Serikali itoe *commitment* nzuri ya kutusaidia. Natoa hoja.

MWENYEKITI: Hakuna aliyeunga mkono lakini.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sichalwe hamna, si hao watatu tu, hata kumi hawajafika. Haya, wanne tu. Sasa wanne tunafanyaje jamani? Hah, mnaongezeka tena watano, hamjafika kumi bado. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Sichalwe, naomba tuwaachie tu Serikali wakaifanyie kazi kwa sababu hoja yako ni ya msingi na watu wengi wamenufaika kutokana na kazi hiyo, lakini pia mamilioni ya Watanzania wanaweza kuangamia endapo Serikali haitakuwa na uhakika wa kitu ambacho kinafanyika. Kwa hiyo, naomba tuiachie Serikali iende ikatafakari, halafu tutajua nini cha kufanya. Katibu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 449,260,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh. 1,116,510,000
Kifungu 1004 - <i>Government Communication Unit</i>	Sh. 207,468,000
Kifungu 1005 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 264,568,900
Kifungu 1006 - <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 211,348,000
Kifungu 1007 - <i>Management Information System</i>	Sh. 309,082,000
Kifungu 1008 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 212,319,000
Kifungu 2001 - <i>Industry</i>	Sh. 9,910,784,164
Kifungu 2002 - <i>Small and Medium Enterprises Division</i>	Sh. 6,113,874,672
Kifungu 3001 - <i>Commerce</i>	Sh. 1,360,740,000
Kifungu 4002 - <i>Commodity Market Develop</i>	Sh. 26,328,481,468
Kifungu 5001 - <i>Investment Development Division</i>	Sh. 3,585,094,121
Kifungu 5002 - <i>Economic Empowerment Private Sector Development</i>	Sh. 2,653,548,912

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 44 – Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Kifungu 1001 - <i>Administration & Human Resources Management</i>	Sh. 1,600,000,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh. 7,993,600,000
Kifungu 2001 - <i>Industry</i>	Sh. 17,461,219,000
Kifungu 2002 - <i>Small and Medium Enterprises Division</i>	Sh. 3,742,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, ndc – KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge sasa naomba namwita mtoa hoja ili aweze kutoa hoja yake karibu sana Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

T A A R I F A

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na hoja imeungwa mkono. Sasa moja kwa moja kwa mujibu wa kanuni nitalihoji Bunge. wanaokubaliana na hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na bajeti yake ipitishwe. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waliokubali wameshinda na hoja hii imepitishwa. Nawashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya Waheshimiwa Wabunge kuanzia siku ya Ijumaa, naamini kabisa matokeo ya leo yametokana na jinsi ambavyo mmepitia vitabu vyote vya bajeti kuanzia Ijumaa, Jumamosi na Jumapili yake na ndiyo maana leo tumeweza kuhitimisha mapema kabisa. Pia hii ni faraja kuona kwamba Wizara yetu imeungwa mkono na Wabunge wote, wengi wametoa ushauri mzuri sana.

Naipongeza Kamati na Wabunge wote ambao wamechangia moja kwa moja na kwa maandishi. Naamini kabisa Mheshimiwa Waziri na timu yako mtayapokea maoni yote ya Wabunge ambayo yametolewa na kuyaangalia kwa umakini wake na baadaye kuweza kutekeleza yale ambayo yataweza kusaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Pia mwanzo wa bajeti moja ni mwendelezo wa bajeti nyingine, naamini mashauri mengine ambayo yametolewa yataenda kutusaidia kwenye bajeti zinazofuata. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwaombea kila la heri wenzetu Serikalini kupitia Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili yale ambayo yamepitishwa basi muweze kupata bajeti ambayo inastahiki na baadaye tuweze kuendelea na yale ambayo tumeyakusudia kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Basi baada ya kuzungumza hayo machache, nawashukuru tena kwa mara nyingine, nawatakia mapumziko mema na naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 6.50 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 10 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)